SUPA JACKPOT
TZS.1,107,465,397
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



**Magereza** waja na sare mpya kwa wafungwa wanawake

UKURASA 5


ama
ALHAMISI APRILI 27, 2023
AFYA NA MAZINGIRA
Ukurasa 12
MSD inavyokuwa mkombozi Hospitali Rufani mkoa Dodoma, inazaliwa upya
Ukurasa 13
Kamanda Mohamed wa TFS Kanda ya Ziwa asimulia ndani, nje vita vyao kuokoa misitu
Ukurasa 14
SBL yawajibikia jamii kupitia 'Lengo la Sita SDG' maji imfikie mama Handeni
AFYA
Chanjo aliyozindua Rais yajibu makubwa kimataifa, WHO ikimwaga pongezi kuu
Na Yasmine Protace

UKURASA 11


# Nipashe

Alhamisi Aprili 27, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581293

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US




# AKAMATWE

• **Waziri** Mkuu aagiza mwanajeshi aliyedhalilisha ashughulikiwe... *Endelea ukurasa wa 2*



Rais Samia Suluhu Hassan akitazama maendeleo ya mtoto Hamimu Baranyikwa (15), mkazi wa Nyakanazi mkoani Kagera, anayesumbuliwa na maradhi ya ngozi, aliyefika Ikulu, Dar es Salaam jana kumshukuru Rais kwa kugharamia matibabu yake ya miezi sita katika Hospitali ya Taifa Muhimbili. Rais pia alimpa mkono wa Eid. **PICHA: IKULU**

## YALIYOMO


UKURASA WA 4
**MAKAMU ASKOFU ATOA USHAHIDI MAHAKAMANI**
MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Geita imeanza kusikiliza kesi...

UKURASA WA 5
**MSHTAKIWA NYARA ZA JESHI ALITUDANGANYA**
SHAHIDI MT 8726 Sajenti Zamoyoni Mpeta kutoka Jeshi la Ardhini...

UKURASA WA 8
**DPP AAGIZA MAPITIO JALADA KESI UHUJUMU VIGOGO WA TPA**
MKURUGENZI wa Mashitaka (DPP), ametoa maelekezo kuwa jalada la kesi...


## VETA yabuni miwani kuzuia dereva asisinzie

UKURASA 3



MIAKA 59 MUUNGANO...

## CHADEMA na ACT: Ushirikishwaji ni muhimu, sumu uzanzibari, uzanzibara

UKURASA 2

**MICHEZO** RAIS ATAMANI KUIONA YANGA, RIVERS UK.24 **KATUNI** UK.6



Mkuu wa Jeshi la Magereza nchini, Kamishna Jenerali Mzee Ramadhani Nyamka (kulia), akionyesha sare mpya za wafungwa wanawake ikiwemo suruali, blauzi na kofia baada ya kuizindua mjini Mororogoro jana, ambazo zitaanza kutumika leo kwenye magereza yote nchini. Kushoto ni sketi na blauzi sare iliyokuwa ikitumika awali ambayo kwa sasa haitatumika tena. Habari Uk. 5. **PICHA: ASHTON BALAIGWA**

# PM aamuru mwanajeshi anayetuhumiwa kuchukua televisheni ya raia kukamatwa

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa ameagiza kusakwa kwa mwanajeshi maarufu kwa jina la HK anayeishi eneo la Nzuguni, jijini Dodoma anayedaiwa kuchukua televisheni ya kijana aliyemtuhumu kuonekana na simu ya mke wake.

Waziri Mkuu alitoa agizo hilo jana alipokuwa akizungumza na wananchi wa Nzuguni katika maadhimisho ya miradi iliyozinduliwa katika kilele cha sherehe za miaka 59 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, kikiwamo kituo cha Zimamoto na Uokoaji.

Kijana huyo alitoa tuhuma hizo, baada ya Waziri Mkuu kutoa nafasi kwa wananchi kuzungumza kero zinazowakabili ili waweze kupata msaada.

Alipopata nafasi hiyo, alidai mwanajeshi huyo aliyemtaja kwa jina maarufu la HK, kunyanyasa vijana wa eneo hilo na yeye akiwamo kwa kuchukuliwa TV yake kwa madai kuwa kuna mtu amemuambia kuwa amemuona na simu ya mke wake.

"Alikuja nyumbani kupekua vitu vya nyumbani kwangu zikiwamo nguo za ndani za mke wangu kwa kuziinua huku akizinyanyapaa, alipokosa simu aliamua kubeba TV na kuondoka nayo na jana amenipigia simu kuniambia kuwa kero yangu hata nikipeleka kwa Rais Samia haitatatulika...naomba Waziri Mkuu nisaidiwe afuatiliwe," alilalamika.

Waziri Mkuu alimuagiza Kamanda wa Polisi mkoani hapa, Martin Otieno, kumsaidia kijana huyo na kumtafuta mwanajeshi huyo ili akamatwe.

"Pia nitazungumza na CDF (Mkuu wa Majeshi) kama anavyoeleza kijana huyu kama ndivyo kamanda yeyote wa jeshi lolote hapaswi kuwafanya hivyo Watanzania, jeshi lipo kwa ajili ya kuwalinda wao, maisha yao, vifaa vyao na mali zao zinakuwa salama sio kwenda kuchukua mali zao," alionya.

"Huyo kijana apatikane na kama atakataa tutapata taarifa zake kwenye kikosi alipo na tutamtafuta CDF atatupa mawasiliano ili tujue kwanini amechukua TV ya huyu kijana.

Huyu kijana apewe ushirikiano anaweza kupata matatizo na huyo kamanda akisikia ametamkwa hadharani, huyu kijana alindwe asipate madhara."

Alisema taarifa ya kijana hiyo ichukuliwe kama taarifa kamili na ifanyiwe kazi ili apate haki yake ya msingi.

Katika hatua nyingine, Majaliwa alisema serikali imetenga Sh. bilioni 9.93 mwaka ujao wa fedha 2023/24 kwa ajili ya kukamilisha miradi ya ujenzi wa vituo saba vya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji vitakavyojengwa mikoa ya Songwe, Simiyu, Kagera, Njombe, Manyara, Katavi na Geita.

Akifungua vituo vya kisasa vya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji vya Nzuguni na Chamwino, mkoani hapa vilivyogharimu zaidi ya Sh. bilioni 2.3, Majaliwa alisema

ujenzi wa vituo hivyo pamoja na upatikanaji wa vitendea kazi vya kutosha vitasaidia usalama wa wananchi na mali zao unakuwapo.

"Kukamilika kwa miradi hii kutasaidia kusogeza huduma za Zimamoto na uokoaji karibu zaidi na wananchi na kuongeza ufanisi wa utoaji huduma na uokoaji kwa kufika eneo la tukio kwa wakati," alisema.

Majaliwa alisema, miradi mingine inayotekelezwa na serikali ni ujenzi wa ofisi ya kisasa za Jeshi la Zimamoto Temeke, Dar es Salaam, vituo vya polisi vya daraja A vya Kigamboni Dar es Salaam na Wanging'ombe, mkoani Njombe, Ofisi za Uhamiaji za mikoa ya Lindi na Geita na Ofisi za Makamanda wa Polisi katika mikoa ya Kusini Unguja na Kaskazini Unguja ambayo itagharimu zaidi ya Sh. bilioni 16.

Waziri Mkuu alilitaka jeshi hilo lisimamie vizuri matumizi ya fedha za miradi zinazotolewa na serikali ili kuharakisha mchakato wa utekelezaji wa miradi hiyo muhimu kwa kuhakikisha kuna uwiano kati ya ujenzi wa miradi na thamani halisi ya fedha inayotolewa na serikali.

Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Yusuf Masauni, alisema wapo kwenye hatua za mwisho za ununuzi wa vifaa vya jeshi hilo na watanunua hadi helikopta za kuzimia moto.

Awali, Kamishna Jenerali wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, John Masunga, alisema serikali imenunua boti za uokoaji majini, kuwezesha kupatikana kwa mkopo wa masharti nafuu wa Euro milioni 4.9 kutoka Serikali ya Austria kwa ajili ya ununuzi wa magari 12 ya kuzima moto ikiwamo mawili yenye ngazi kwa ajili ya majengo marefu.

# CHADEMA na ACT: Ushirikishwaji ni muhimu muungano

**Na Waandishi Wetu**

JANA ilitimu miaka 59 kamili tangu Tanganyika na Zanzibar ziungane na kuwa Taifa moja la Tanzania.

Ingawa sherehe za kitaifa kuadhimisha Miaka 59 ya Muungano zilifutwa na Rais Samia Suluhu Hassan, baadhi ya vyama vya upinzani viliitumia siku hiyo kupaza sauti kuhusu matamanio yake.

Baadhi ya hoja zao ni kutaka kuwapo mjadala wa kitaifa utakaoshirikisha wananchi wa pande zote mbili kuangalia vipengele ambavyo ni kero ili viboreshwe na kupata mwafaka kitaifa.

Ni hoja kutoka kwa Waziri Kivuli wa Katiba na Sheria wa Chama cha ACT-Wazalendo, Victor Kweka, aliyeiambia Nipashe kuwa wanaona ipo haja kuwe na majadiliano hayo anayoamini yataleta mwafaka wa kitaifa kwa hoja zenye mawazo kinzani.

Alisema muungano ni nyenzo imara ya kuzifaidisha nchi zilizoamua kuungana ili kuimarisha nguvu na kunufaika kwa usawa bila kuwa na malalamiko kutoka kwa wananchi wake.

Mkurugenzi wa Mawasiliano, Itikadi na Mambo ya Nje wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), John Mrema, alisema kumekuwa na malalamiko kutoka kwa wananchi wa pande zote mbili yanayoonyesha kutoridhishwa na baadhi ya mambo.

Alisema ili kuuboresha muungano, serikali haina budi kuharakisha mchakato wa kupatikana Katiba mpya kwa kurekebisha kero zinazolalamikiwa na wananchi kuhusu suala hilo, ili kila upande ufurahie matunda ya kuwapo kwake.

Alitolea mfano kuwa, baadhi ya wananchi kutoka Tanzania Zanzibar wanalalamikia mawaziri wengi wanajiita wa muungano ilhali uhalisia ni wa upande mmoja.

"Ni wakati mwafaka sasa serikali iwaulize wananchi wake kuwa wanataka muungano wa aina gani kwa kuwa hao ndio watakaotoa majibu mazuri" alishauri.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Selemani Jafo, jana aliwahimiza watanzania kuuenzi muungano kwa kudumisha amani.

Alitoa kauli hiyo mkoani Iringa wakati wa maadhimisho ya Miaka 59 ya Muungano, akisema kuwa matunda yake yanaonekana kutokana na kuwa imara na wa mfano duniani kulinganisha na nchi zingine zilizowahi kuungana na hatimaye kutengana.

Alisema kuwa kupitia Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, wananchi wanaishi kwa amani na mshikamano, na serikali inatekeleza miradi ya maendeleo kwa ajili ya wananchi wa pande zote mbili za Muungano.

"Ndugu zangu tuna kila sababu ya kujivunia na kutembelea kifua mbele," alisema.

Waziri Jafo pia aliupongeza uongozi wa mkoa huo kwa kufanya vizuri katika utunzaji wa mazingira ambao ni ajenda muhimu katika mustakabali wa nchi.

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Adam Malima, katika maadhimisho ya mkoa huo yaliyofanyika wilayani Kwimba alisema upo umuhimu wa elimu ya muungano kuwekwa kwenye mtaala wa elimu.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, aliiagiza Manispaa ya Singida kuweka askari mgambo kwenye mitaa yote ya mji kwa ajili ya kuwakamata watu wanaotupa taka ovyo na asilimia 20 ya faini itakayotozwa walipwe mgambo.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme, aliwataka Watanzania kuendelea kuwaenzi waasisi wa muungano kwa kuwa ndani ya miaka 59, yamekuwapo maendeleo makubwa katika sekta za afya, elimu, afya na miundombinu.

**RAIS SAMIA**

Katika siku hiyo ya muungano, Rais Samia alikutana na kuzungumza na mtoto Hamimu Baranyikwa (15), mkazi wa Nyakanazi mkoani Kagera anayesumbuliwa na maradhi ya ngozi.

Mtoto huyo alikwenda Ikulu jana kwa ajili ya kumshukuru Rais Samia kwa msaada wa matibabu aliompatia katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH).

Rais alimwona mtoto huyo kwa mara ya kwanza Oktoba 16 mwaka jana wakati wa ziara yake mkoani Kagera na kuagiza apatiwe matibabu baada ya kuhangaika kwa muda mrefu.

Baada ya kuwasili Ikulu, mtoto huyo ambaye hakuwa na uhakika kwamba aliyekuwa anazungumza naye ni Rais wa Tanzania hadi alipohakikishiwa na Samia mwenyewe, alimweleza Rais kwamba sasa anaendelea vizuri na kumshukuru kwa msaada wake.

"Si ulisema unataka kuniona! Ndio mimi, uliomba unataka kuniona, nikawaambia mleteni anione," Rais Samia alisema huku mtoto huyo akijibu "ahsante, nimefurahi kukuona".

***Imeandaliwa na Jenifer Gilla, Romana Mallya na Halfani Chusi (DAR), Thobias Mwanakatwe (SINGIDA), Marco Maduhu (SHINYANGA) na Vitus Audax (MWANZA).**

# VETA yabuni miwani ya kuzuia dereva asisinzie

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KATIKA kukabiliana na wimbi la ajali za barabarani, Chuo cha VETA Dodoma kimebuni mfumo maalum wa kielektroniki wa kudhibiti ajali ikiwamo miwani itakayomdhibiti dereva wa basi asisinzie.

Akizungumza jana na waandishi wa habari kwenye maonesho ya wiki ya ubunifu yanayofanyika jijini hapa, mwalimu wa chuo hicho, Yusuph Haule, alisema ubunifu huo unakwenda kutatua wimbi hilo hasa kwa madereva wa mabasi na malori wanaosinzia nyakati za usiku.

"Madereva wengi wanasafiri umbali mrefu ili kudhibiti ajali zinazotokana na usingizi, tumetengeneza miwani ya kielektroniki ambayo itakuwa inampa taarifa dereva kuwa anasinzia kwa hiyo tumeweka vitu vya kielektroniki kwenye mfumo ambavyo vinahesabu mikonyezo."

"Mwanadamu ambaye ni mzima anakuwa na mikonyezo ya macho (kufumba na kufumbua) mara 15 hadi 25 kwa dakika moja. Mfumo huu tumetengeneza kwa kuweka controller ambazo zimepewa akili ambayo imepangiliwa na kompyuta kwa ajili ya kudhibiti mikonyezo ya macho."

"Macho ya dereva yakienda kinyume na mfumo ulivyowekwa, kwenye mfumo tumeweka dereva akisinzia atapata taarifa mara tano mfululizo na asipoikia moja kwa moja mfumo utapunguza spidi hadi kufikia 20 kwa kuwa tunategemea spidi hiyo si hatarishi hata ikitokea akalala kabisa madhara makubwa hayatakuwapo kama akisinzia kwenye mwendo kasi," alisema.

"Kwenye miwani tumeweka sensor ambayo inaangalia mikonyezo ya macho kulingana na ilivyopangiliwa tumeweka mikonyezo kuanzia 15 hadi 30, na pale dereva anapoanza kusinzia atasikia sauti ambayo itasikika kwa abiria wote pia itasema hivi; 'dereva unasinzia kwa usalama wa abiria na watumiaji wengine wa barabara simamisha gari lako' ujumbe huu utarudia mara kadhaa."

Haule alisema gari itapunguza kasi kulingana na mfumo wa umeme uliopo kwenye gari, lakini utaunganishwa na mfumo wa mafuta kwenye gari.

"Miwani yetu inaanza kufanya kazi mara moja tu baada ya kuwasha gari na mfumo pia unamkumbusha dereva kuvaa miwani, kwa sasa miwani iliyopo ni kwa usiku tu, lakini tunatengeneza iwe ya muda wote," alisema.

Kadhalika, alisema mwendelezo wa mfumo huo ni kuboresha kulingana na visababishi vya ajali ikiwamo ulevi.

"Kitawekwa kifaa maalum ili dereva anapoanza safari asiwe amelewa, tumeshaagiza vifaa na hivi karibuni vitakuja na tutakamilisha mfumo matarajio yetu sisi kuhakikisha tunakuwa na mfumo mzima wa kudhibiti viashiria vyote vya ajali," alisema.

Alisema wao wamekuja na mfumo unaozungumza kwa sauti na kuwapa taarifa abiria kufunga mikanda na kumtaka dereva kupunguza spidi.

Akizungumza kwenye siku maalum ya Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) kwenye maonesho hayo, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, alipongeza ubunifu huo ambao utasaidia kupunguza tatizo la ajali nchini.

"Kuna kijana mmoja kwenye banda la VETA ametengeneza miwani ambayo dereva akivaa kama akisinzia inamkumbusha kwa sauti kwa kumwambia asisinzie, tunafahamu kwamba Serikali imekuwa ikihangaika muda mrefu jinsi gani ya kuzuia ajali sasa kijana wa kitanzania ametupatia ufumbuzi tunaimani teknolojia hiyo itaendelea kitumika kupunguza ajali nchini," alisema.

Naye, Mkurugenzi wa Mafunzo ya Ufundi Stadi VETA, Abdallah Ngodu, alisema katika siku hiyo wameonesha ubunifu mbalimbali na kufanya mdahalo kwa ajili ya umuhimu wa elimu na mafunzo ya ufundi stadi.

Mkurugenzi wa Idara ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu, Prof. Maulilio Kipanyula, alisema katika maonesho ya wiki hiyo ya ubinifu kutakuwa na siku maalumu kwa ajili ya VETA na Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania (TAEC) kutokana na uwekezaji mkubwa uliofanywa na serikali katika ufundi na kuzalisha wabunifu wenye uwezo wa kuingiza sokoni bunifu zinazotatua kero za jamii.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo Wilaya ya Iringa**
**Kituo cha Bomani Mkoa wa Iringa**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU ALFRED THOMAS KINGWE**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI WA MIRATHI YALIYOLETWA NA 37/2023**
**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 28 mwezi 04 mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;** Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwaWosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa Imetolewa leo tarehe 18 mwezi 4 mwaka 2023



**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**DEED POLL CHANGE OF NAME**
**(UNDER CAP.117, R.E.2002)**
**By this deed 1, MWANAHAJI ISA PILI an adults, Muslim and resident of MKUZO, do solemnly state as follows:**

1. That, 1 hereby absolutely renounce and abandon the use of former name of MWAWAHAJI ISSA PILLI, PILI MWANAHAJI ISA and in place thereof do assume and adopt the name of MWAWAHAJI ISA PILI
2. That ,in pursuance of such change of name as aforesaid I do hereby declare that, I shall at all material times hereinafter in all records , deed and instruments in writing and in actions , proceedings and transactions and upon all occasion whatsoever usa and sign the name of MWANAHAJI ISA PILI as the name in place of the former name of MWAWAHAJI ISSA PILLI, PILI MWANAHAJI ISA.
3. That, I further authorizes and request all people to designate and address me by such assumed name of MWANAHAJI ISA PILI.

I make this declaration consciously believing the name to be in accordance with the provisions of Oaths and Statutory Act, 1966.

Signed and Addressed by the said
MWANAHAJI ISA PILI
formally known as
MWAWAHAJI ISSA PILLI,
PILI MWANAHAJI ISA
this 9 day of December, 2022



BEFORE ME:
NAME: G. K. KIDIMBO
SIGNATURE:
ADDRESS:
COMMISSIONER FOR OATH



**KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI**

**ALIFU JUMA MAKANG'A**

anatangaza kupotelewa na kadi ya BAJAJ yenye namba za usajili MC 924 DAC YENYE CHASES NAMBA: MD625AE37M1C00212. Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa polisi.

Taarifa ya polisi RB. Namba **IRI/IRI/RB/140940/2023**





# Makamu Askofu atoa ushahidi kortini kuvunjwa kanisa kuu

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Geita imeanza kusikiliza kesi inayomkabili Elpidius Edward (26), anayekabiliwa na mashataka mawili ya kuvunja Kanisa Kuu Jimbo Katoliki Geita na kuingia ndani na kuharibu vitu mbalimbali vyenye thamani ya Sh. milioni 48.286, mali ya Kanisa Kuu Jimbo Katoliki la Geita.

Mshtakiwa huyo alipandishwa kizimbani mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi wa Mahakama hiyo, Johari Kijuwile na aliposomewa mashtaka yake alikana kuhusika na makosa yote mawili na yuko mahabusu katika Gereza la Wilaya ya Geita kutokana na kukosa wadhamini.

Upande wa Mashtaka, uliongozwa na Wakili wa Serikali, Venance Mkonongo. Kwa jana kulikuwa na shahidi mmoja aliyekuwa tayari kuwasilisha ushahidi.

Shahidi huyo, Makamu Askofu wa Kanisa Kuu Jimbo Katoliki Geita, Elias Masolwa akiongozwa na Wakili wa Serikali Mkonongo, alidai mahakamani huko kuwa Febuari 26 mwaka huu, majira ya saa nane usiku, alipigiwa simu na Padri Slas Kato na kupewa taarifa kwamba, kuna mtu alikuwa ameingia kanisani na kuharibu vitu mbalimbali.

Masolwa alidai kuwa baada ya kupewa taarifa hiyo, alikwenda hadi kanisani na kufungua mlango wa kanisa hilo na alipoingia ndani, alikuta askari wawili wa kanisa hilo wakiwa wamemfunga mtuhumiwa mikono kwa kutumia mkanda.

Alidai kuwa baada ya kuona mtuhumiwa huyo ameshikiliwa na askari wa kanisa hilo, alipiga simu Kituo cha Polisi Geita na polisi walifika na kumchukukua mtuhumiwa huyo na kuondoka naye na baadaye askari polisi walikwenda tena kanisani, safari hii wakimwuliza thamani ya vitu vilivyoharibiwa.

Makamu Askofu huyo alidai kuwa ndani ya kanisa hilo kulikuwa na damu na uharibifu wa vitu mbalimbali vyenye thamani ya Sh. milioni 48.286 na aliorodhesha vitu vyote na kuandika kwenye karatasi kisha akawakabidhi askari polisi.

Alisema kuwa baada ya kuwakabidhi polisi orodha ya vitu vilivyoharibiwa na thamani yake, askari hao waliondoka na kumwahidi kuendelea na upelelezi wa tukio hilo.

Hakimu Kijuwile alimwuliza mshtakiwa huyo kama ana maswali ya kumuliza shahidi wa upande wa Jamhuri, mshtakiwa akajibu alikuwa nayo.

Sehemu ya mahojiano yao mahakamani ilikuwa:

**Mshtakiwa:** Kama wewe ulikuwa na funguo za kanisa, hao askari waliingiaje ndani ya kanisa?

**Shahidi:** Askari walipitia pale wewe ulipoingilia.

**Mshtakiwa:** Kanisa hilo lilikuwa na walinzi wangapi?

**Shahidi:** Kanisa lilikuwa na mlinzi mmoja.

**Mshtakiwa:** Mtuhumiwa alikuwa na hali gani?

**Shahidi:** Nilimwona mtuhumiwa amefungwa mikono kwa mkanda.

**Mshtakiwa:** Ulimwona mtuhumiwa akiwa na kitu?

**Shahidi:** Nilimwona mtuhumiwa akiwa amefungwa mikono kwa kutumia mkanda.

Baada ya mshtakiwa kumaliza kumuuliza maswali shahidi wa Upande wa Jamhuri, Wakili wa Serikali Mkonongo aliomba tarehe nyingine kwa ajili ya kuendelea kusikiliza mashahidi wengine waliobaki.

Hakimu Kijuwile alikubaliana na ombi hilo na kuahirisha kesi hiyo hadi Mei 10 mwaka huu kwa ajili ya kuendelea kusikiliza mashahidi wengine.

# DC kumaliza utata wa kokoto

**Na Ambrose Wantaigwa,**

**RORYA**

MKUU wa Wilaya ya Rorya mkoani Mara, Juma Chikoka, leo anatarajiwa kumaliza utata uliotokana na uchimbaji wa changarawe katika mlima ulioko katikati ya kijiji kwa ajili ya ukarabati wa barabara.

Jumatatu ya juma hili, Chikoka alizuru katika Kijiji cha Rabuor, Kata ya Rabuor, na kuunnda kamati ya watu saba aliyoipa jukumu la kufuatilia malalamiko ya wananchi waliopinga uchimbaji huo wa kokoto unofanywa na mkandarasi anayejenga barabara ya Kuruya-Utegi.

Kamati hiyo inayoundwa na wataalamu kutoka ofisi mbalimbali zikiwamo Wakala wa Barabara (TANROADS), Idara ya Mazingira, Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya na wananchi wa kijiji hicho, ilipewe siku mbili, juzi na jana kufanya ufuatiliaji huo na kuwasilisha taarifa kwa Mkuu wa Wilaya huyo leo.

Barabara hiyo yenye urefu wa kilomita 47 inajengwa kwa kiwango cha changarawe kwa gharama ya zaidi ya Sh. milioni 860 na mkandarasi Jonta Investment.

Wananchi wa Kijiji cha Rabuor walilalamika kwa Mkuu wa Wilaya uchimbaji wa malighafi ya ujenzi katika mlima huo haukuwa shirikishi na kinachoendeleo kinatishia uhai wa mlima huo ambao umekuwa ukitumiwa kwa masuala kadhaa yakiwamo matambiko ya kimila.

James Waritu, mkazi mwingine wa kijiji hicho, alidai uamuzi uliofanywa na baadhi ya viongozi wa serikali ya kijiji kuruhusu mkandarasi huyo kuchimba udongo na kokoto katika mlima huo haukuwashirikisha wakazi wa kijiji hicho, hivyo kuomba uamuzi huo ubatilishwe na utaratibu uanze upya.

Julius Nono, mwanakijiji na mkazi wa eneo hilo, alisema mlima huo pia umezungukwa na taasisi mbalimbali yakiwamo makanisa, shule za msingi na sekondari, hivyo uchimbaji huo unahatarisha kuwapo wa taasisi hizo.

Kufuatia malalamiko hayo, Mkuu wa Wilaya aliamua kuunda timu hiyo na kutoa muda wa siku mbili kufuatilia undani wa hoja hyo, pia wafanye upembuzi kujua athari za kimazingira, kijamii na kimila na kisha kutoa ushauri wa nini kifanyike.

EAST AFRICAN
CRUDE OIL
PIPELINE

**MAOMBI YA KUONESHA NIA YA UTOAJI WA HUDUMA ZA USANIFU NA UTEKELEZAJI WA UREJESHAJI WA MAKAZI NA MAZALIO YA MATUMBAWE KWA AJILI YA VIUMBEHAI WA BAHARINI NA MIPANGO YA UREJESHAJI WA MAZINGIRA KATIKA HALI BORA ZAIDI MKOANI TANGA: KUMBUKUMBU NA: REQ-00000197**

Kampuni ya Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) Ltd, ("EACOP LTD") inakaribisha kampuni zenye uzoefu na weledi wa kutosha kuonesha nia ya kutoa huduma ya urejeshwaji wa Makazi na Mazalio ya Matumbawe kwa ajili ya viumbehai wa baharini na mipango ya kurejesha mazingira katika hali bora zaidi mkoani Tanga katika Mradi wa EACOP.

Mradi wa EACOP unajumuisha shughuli za ujenzi na uendeshaji wa bomba la kusafirisha Mafuta ghafi lililofukiwa chini ya ardhi linalokatisha mipaka ya nchi mbili (Tanzania na Uganda) kwa ajili ya kusafirisha Mafuta ghafi kwenda masoko ya kimataifa. Bomba litaanzia Kabaale katika Wilaya ya Hoima, nchini Uganda, mpaka rasi ya Chongoleani, Mkoani Tanga, nchini Tanzania. Urefu wa bomba ni kilomita 1,443, kati yake kilomita 1,147 zitakuwa nchini Tanzania.

**MAELEZO MAFUPI KUHUSU HUDUMA**
Miundo mbinu ya EACOP katika rasi ya Chongoleani inajumuisha Kituo cha kuhifadhi Mafuta (MST), magati mawili, Kituo cha Kupakua mafuta (LOF). Eneo dogo la Matumbawe kwa ajili ya makazi na mazalio ya viumbehai wa baharini litaguswa na shughuli za ujenzi na uendeshaji wa gati. Mpango kazi wa Bayoanuai (BAP) unaoeleza takwimu za awali za maeneo yaliyoguswa na mradi umeandaliwa.

Kampuni/mshauri wa kitalaamu au taasisi yenye weledi inahitajika kwa ajili ya kusanifu na kutekeleza mpango wa urejeshaji wa makazi na mazalio ya Matumbawe kwa ajili ya viumbehai wa baharini na mipango ya kurejesha mazingira katika hali bora zaidi katika eneo la maji ya kina kifupi kwa kuzingatia vigezo na mbinu bora, kujifunza kutokana na mipango iliyopo katika eneo hilo, na kwingineko katika ukanda huu au duniani kote. Mbinu inayopendekezwa ni pamoja na urejeshaji wa ekolojia ya matumbawe kijamii (CBECR) unaohusisha wadau wa ndani na makundi mengine kutoka eneo hilo ikiwa ni pamoja na jamii za wenyeji, taasisi za serikali na Mashirika ya kiraia. Maamuzi ya urejeshaji yatapaswa kuzingatia data za kisayansi ili kuweka mizania sawa kulingana na hali iliyopo ya kijamii na kimazingara na mabadiliko tarajiwa ya baadaye.

**VIGEZO MUHIMU:**
**Makampuni au taasisi zinzoonesha nia zinakaribishwa kutuma maombi na kuambatanisha nyaraka zifuatazo.**

- Uthibitisho wa usajili wa taasisi ambayo shughuli zake zinahusisha ushirikishwaji wa jamii (kama vile ushiriki wa jamii katika urejeshaji wa makazi katika Matumbawe kwa ajili ya viumbehai wa baharini) nchini Tanzania.
- Taarifa fupi kuhusu uzoefu na uwezo wa kusanifu na kutekeleza mpango wa urejeshwaji wa makazi na mazalio ya Matumbawe, kwa kufanya kazi na kujenga uwezo wa jamii ya watu wa pwani, kuanzisha vitalu vya matumbawe, kufanya utafiti jaribizi kuhusu matumbawe, kufuatilia na kutathimini hali ya matumbawe na kubaini maneneo yanayofaa kwa urejeshaji wa makazi katika matumbawe kulingana na sifa za kimaumbile, kihaidrolojia na kibayolojia.
- Mifano ya shughuli zinazoonyesha uzoefu wa kufanya shughuli ya urejeshaji kama hii, ambazo taasisi imetekeleza kwa kipindi cha hivi karibuni: ndani ya miaka mitano .
- Wasifu wa wafanyakazi muhimu watakaohusika katika mradi ikiwa ni pamoja na vyeti vya lazima vya wahudumu na viwango vya elimu, pamoja na uzoefu na uwezo wa kutoa huduma zinazotakiwa.
- Leseni halali, kama ipo, kutoka mamlaka ya ndani ya nchi husika kwa ajili ya utoaji wa huduma husika.
- Uthibitisho wa kusajiliwa na Mamlakaya Mapato Tanzania (TRA) na Cheti cha Mlipa kodi cha mwaka wa hivi karibuni.
- Waombaji wanasisitizwa sana kuhakikisha kuwa wamejisajili kwenye kazidata ya EWURA (LSSP) ya Watoa Huduma za Ugavi wa Ndani, wakati wa kuwasilisha maombi ya kuonesha nia,
- Kukidhi vigezo na Kanuni za watoa huduma Wazawa za mwaka 2017.
- Uwezo wa kifedha wa kutoa huduma zinazohitajika ikiwa ni pamoja na kuwasilisha hesabu za fedha za miaka mitatu iliyopita
- Uthibitisho kutoka kwenye mfumo wa Usimamizi wa **QHSE**, taasisi na mchakato kulingana na Viwango vya Ndani na vya Ki-Sekta vinavyotumika kwa kazi kama hii.
- Uthibitisho wa sera ya kupinga vita rushwa, ufisadi, na kuzingatia Haki za Binandamu.

Kampuni zenye nia, uwezo na rasilimali za kutosha kutekeleza shughuli zilizotajwa hapo juu zinakaribishwa kutuma maombi pamoja na kuambatanisha nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe ya **procurement.tz@eacop.com**, (ukubwa wa barua pepe usizidi **20Mb**). Maombi yatumwe kabla au mnamo tarehe **12 May 2023**, **saa 11 jioni** saa za Afrika Mashariki. Kichwa cha Barua pepe kiwe **00000197** - Utoaji wa huduma ya urejeshwaji wa Makazi katika Matumbawe kwa ajili ya viumbehai na mipango ya kurejesha mazingira katika hali bora zaidi mkoani Tanga katika Mradi wa EACOP
Maombi yote ya kuonesha nia yawe kati ya kurasa 10 hadi 20
Maombi yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kingereza

**Muhimu:** Kampuni ya EACOP LTD itapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na makampuni yenye nia kulingana na EOI hii na kisha kufanya tathmini kwa kutumia vigezo vya ndani ili kubaini makampuni yatakayojumuishwa kwenye orodha ya (Makampuni) ya awali yaliyokidhi vigezo. Makampuni yaliyofuzu hatua za awali pekee ndiyo yatakayopewa mwaliko wa zabuni, kwa kutia saini Mkataba wa Kutunza Siri (NDA), kama mwendelezo wa wito wa mchakato wa utoaji wa zabuni. Kampuni ya EACOP LTD inayo haki ya kufanya maamuzi yake ya kuchagua au kukataa kampuni na kubaki na maamuzi yake pasipo kutoa sababu kwa kampuni husika

217397802

## HABARI KITAIFA

ASKARI JWTZ ADAI KORTINI...

# Mshtakiwa nyara za jeshi alitudanganya nyumba anayoishi, tukambana, akaitaja

**Na Grace Gurisha**

SHAHIDI MT 8726 Sajenti Zamoyoni Mpeta kutoka Jeshi la Ardhini (Kibaha), ameeleza mahakamani namna alivyomkamata mfanyakazi wa SumaJKT, Michael Fumbuka na vifaa vya jeshi na alivyowadanganya wakaenda kufanya upekuzi kwenye chumba cha rafiki yake badala ya chumba chake.

Sajenti Mpeta alidai hayo juzi mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Richard Kabate wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam wakati akitoa ushahidi dhidi ya Fumbuka anayetuhumiwa kukutwa na kombati za jeshi na nyara za serikali.

Alidai kuwa awali alikuwa Kitengo cha Upelelezi cha Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) Makao Makuu ya Vikosi vya Chini (Upanga, Dar es Salaam).

Alidai kuwa akiwa kwenye ofisi hiyo, mkuu wake wa kazi alimweleza kuwa wamepata taarifa kutoka Kikosi 514 cha Makambako kuwa kuna kijana anajihusisha na nyara za serikali na kuuza kombati za jeshi. Shahidi huyo alidai kuwa baada ya taarifa hiyo, yeye akiwa na Koplo Mapote, Fakri na Rasilia walianza kumu la kumfutilia kijana huyo (Michael Fumbuka) anayetuhumiwa kujishughulisha na biashara hizo.

Alidai kuwa taarifa hizo zote walizipata kutoka kwa Elia Kiwili ambaye alibanwa kwenye Kikosi 514 kilichoko wilayani Sumbawanga na kumtaja Fumbuka kuwa walikuwa wanashirikiana kufanya biashara hizo.

Alidai kuwa baada ya kumkamata huko Buguruni, walielekezwa wampeleke mtuhumiwa huyo katika Kikosi cha CJU kilichoko Wilaya ya Temeke, Dar es Salaam kwa ajili ya maelezo ya awali na baadaye alielekezwa amtoe kambini huko, ampeleke Kituo cha Polisi cha Kigogo.

Alidai kuwa Oktoba 28, 2021, akiwa ofini, alipewa taarifa kuwa anaombwa kwenda Kituo Kikuu cha Polisi kwa ajili ya kufanya upekuzi nyumbani kwa mtuhumiwa.

Shahidi huyo alidai kuwa mtuhumiwa huyo aliwaeleza kuwa anakaa Buguruni, walipofika walimkuta mama mwenye nyumba Jane Brown wakajitambulisha kwake na kumweleza kuwa wanataka kufanya upekuzi kwenye chumba cha Fumbuka kama watakuta nyara za serikali za kijeshi. Alidai kuwa walipopekua walikuta hati ya ujenzi yenye jina la Prisila, wakati wanaendelea na upekuzi walibaini kuwa chumba hicho si cha mtuhumiwa na baada ya kumbana, alidai kuwa chumba hicho ni cha rafiki yake, yeye anaishi Vingunguti.

"Tulipofika tulimkuta mama mwenye nyumba Lucy Mlai, katika kupekua tulikuta radio call moja aina ya Motorola, mkanda wa kuvaa JWTZ, muhuri wa moto wa Makao Makuu JKT, muhuri wa Makongo, cheti cha JKT cha Michael Fumbuka na barua ya utambulisho wa kumaliza mgambo Sumbawanga," alidai.

Alidai Novemba 8, 2021 akiwa ofisini, alipewa taarifa kutoka Kituo Kikuu cha Polisi, akitakiwa aende kuthibitisha vyeti na mihuri aliyokamatwa nayo mtuhumiwa na alikwenda Dodoma Makao Makuu ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) kwenye ofisi ya usalama, akawakabidhi kwa ajili ya uthibitisho kama ni vyenyewe au la.

Alidai kuwa baada ya hapo walifanyiwa kazi na alielekezwa kwamba avirudishe vitu hivyo Kituo Kikuu cha Polisi Dar es Salaam.

Kesi hiyo iliahirishwa hadi Mei 10 mwaka huu kwa ajili ya kuendelea kusikilizwa. Mshtakiwa anakabiliwa na mashtaka sita.

# Sare mpya kwa wafungwa zaja

**Na Ashton Balaigwa**

JESHI la Magereza limelazimika kubadili sare zake kwa wafungwa wanawake waliokuwa wakitumia sketi, blauzi na kitambaa kichwani na sasa watatumia suruali, blauzi na kofia.

Uamuzi huo umechukuliwa baada ya jeshi hilo kubaini sare za awali zilikuwa na dosari kadhaa, ikiwa ni pamoja na kuonyesha maumbile yao pindi wanapofanya kazi mbalimbali wanazopangiwa, zikiwamo za nje.

Dosari nyingine iliyotajwa ni sare hizo kuwanyima uhuru, kutositiri maumbile yao na nguo za ndani pindi wanapokaa au kuinama,

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa sare mpya za wafungwa wanawake katika Gereza Kuu la Wanawake Mkoa wa Morogoro, Mkuu wa Jeshi hilo, Kamishna Jenerali Mzee Ramadhani Nyamka, alisema lengo la mabadiliko hayo ni kutimiza jukumu la msingi la urekebishaji wa tabia za wafungwa.

Alisema sare za awali zilikuwa zikiathiri katika malezi ya maadili ndani ya magereza na kwenye jamii, hasa kwa wafungwa wanawake wenye maumbile makubwa.

Kamishna Jenerali wa Magereza baada ya kuzindua sare hizo, aliagiza wakuu wote wa magereza ya wanawake kuhakikisha wafungwa wanawake wanaanza kuzitumia sare mpya ambazo alisisitiza zimezingatia wanaohukumiwa kifungo wakiwa wajawazito na kusitiri maumbile ya kila mfungwa.

Awali Mkuu wa Gereza Kuu la Wanawake Mkoa wa Morogoro, Mrakibu Mwandamizi wa Jeshi la Magereza, Amina Kavilondo, alisema kwa kutambua changamoto za wafungwa wanawake, waliamua kubuni aina ya sare hizo ili kukabilina na athari zinazoweza kujitokeza kutokana na matumizi ya sare za zamani.

Alisema mchakato wa kubuni sare hizo mpya ulianza Desemba mwaka 2022 na walifanikiwa kushona jozi mbili za sare na kuzifanyia majaribio kwa baadhi ya wafungwa na kuonekana zinakidhi matarajio.



Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Usisubiri kuumwa kujiunga na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya

**MTU** anapokuwa na afya mgogoro hawezi kujiletea maendeleo yake binafsi, ya familia na hata ya taifa lake kwa kuwa kila mara atakuwa ni mtu wa hospitali na kitandani.

Na anapokuwa mgonjwa bila kuwa na pesa ya matibabu tatizo huwa kubwa zaidi kwa sababu huishia kupoteza maisha.

Katika kuhakikisha kuwa binadamu anaishi bila kuwa na shaka anapougua wakati akiwa hana fedha mfukoni ya kujigharamia ni muhimu kwake kujiwekea utaratibu wa kujikatia bima ya afya ili aweze kupata matibabu hata anapokuwa kwenye hali ngumu ya kifedha.

Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), umeweka utaratibu wa kumwezesha kila Mtanzania kupata matibabu kupitia Bima ya Afya anapokuwa mwanachama wa Mfuko huo.

Mfuko huo umeweka utaratibu wa vifurushi vitatu vya Bima ya Afya ya NHIF ambavyo ni mpango unaowezesha mwananchi mmoja mmoja au familia kuchagua na kuchangia huduma za matibabu kabla ya kuugua na kisha kuwa na uhakika wa matibabu kwa kutumia kadi ya bima hiyo bila kikwazo cha fedha.

Vifurushi hivyo vinajulikana kama Najali Afya, Wekeza Afya na Timiza Afya na vimeelekeza kuanzia mwananchi anapotaka kujiandikisha, huduma za kulazwa, za dawa, vipimo vya maabara na uchunguzi, kinywa na meno, uzazi, matibabu ya kibingwa na huduma za upasuaji.

Ingawa kuna baadhi ya watu wanahofu ya kujiunga na bima hiyo kwa madai kuwa wanaweka wasiugue kwa kipindi cha mwaka mmoja na pesa aliyochangia kupotea bure, lakini ni muhimu wakumbuke kuwa lengo la bima hiyo na kuwezesha watanzania kuchangiana gharama za matibabu.

Fedha anayochangia kwenye bima hiyo, inaweza isimsaidie yeye lakini ikamwezesha asiyekuwa na uwezo kupata matibabu na kuokoa maisha yake. Hilo ndilo lengo halisi la bima hiyo.

Kuchangiana katika ugonjwa ili kuokoa maisha ni kitu muhimu kuliko wanavyochangiana kwenye harusi.

Wakati mwingine ugonjwa unaomkabili mtu huwa ni mkubwa na hutumia gharama kubwa ambayo yeye peke yake hawezi kuimudu, lakini bima hiyo humwezesha kupata matibabu kupitia michango inayowekezwa kwenye bima hiyo na kwa kutumia kadi ya uanachama aliyonayo hupata matibabu bila mzigo wa gharama.

Tofauti na mashirika mengine ya umma ambayo hujiendesha kibiashara kwa kuwekeza michango ya wanachama wake, NHIF kazi yake ni kutoa huduma kwa wanachama wake ili kuokoa maisha yao.

Kwa mujibu wa taarifa ya NHIF, magonjwa makubwa ambayo huugharimu mfuko ni saratani, moyo na uchujaji damu (dialysis) ambayo yapo katika kundi la magonjwa yasiyoambukiza.


Mtu anayefanyiwa huduma ya kuchujwa damu, hulazimika kufanyiwa huduma hiyo mara tatu kwa wiki na kama hana kadi ya NHIF inambidi kulipia gharama yote mwenyewe hali inayowashinda watu wenye kipato duni na wasio na uwezo kabisa na hatima yake kupoteza maisha.

Katika kujiunga na Bima ya Afya, mwanachama anatakiwa kuzingatia mambo muhimu kabla ya kujiunga na vifurushi vilivyoainishwa kwenye bima hiyo.

Mwananchi anaweza kujiunga kwa kutumia kitambulisho chake cha Taifa, picha yake moja ya rangi na mwanachama anayetaka kumwandikisha mwenza anatakiwa kuambatanisha picha moja ya mwenza ya rangi, nakala ya cheti cha ndoa pamoja na namba yake ya kitambulisho cha Taifa.

Mwanachama pia anaweza kutoa taarifa za vitendo vya udanganyifu kwa kupiga namba 0800111163. Wananchi ni muhimu kuwa na bima ya afya kuokoa gharama za matibabu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Anthony Gervas

## Muungwana Lazima Nilonge

# Naipongeza serikali kwa wazo kuwekeza viwanda vya mazao ya mifugo Mwanza

**NISEME** hongera kwa serikali mkoani Mwanza kwa uwekezaji wa viwanda viwili vya kuchakata au kusindika nyama za ng'ombe, mbuzi, kondoo, ambavyo vitaweza kuwanufaisha wafugaji na wananchi wengine wa Mkoa wa Mwanza.

Hatua hiyo siyo haba, inatoa fursa kubwa kwa vijana na wananchi wengine kupata ajira viwandani, lakini imewasaidia wafugaji kuwa na soko la uhakika kwa kuuza mifugo yao katika viwanda hivyo.

Peter Kasele, ni Ofisa Mifugo wa Mkoa Mwanza, aliyefafanua kuwapo viwanda hivyo, kuwa ni moja ya hatua zenye tija mkoani hapa, ikiwa viwanda hivyo vipo katika wilaya za Misungwi na Magu.

Anasema takwimu za idadi ya ng'ombe wa asili katika mkoa mzima ni milioni 1,154,174, ng'ombe wa kisasa wako 5,433, mbuzi wa asili ni 565,570, mbuzi wa kisasa 712 na kondoo wako 133,677.

Hiyo ni kwa mujibu wa takwimu za Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2019/2020, maana yake ni hadi kufikia sasa 2023, mifugo hiyo itakuwa imeongezeka zaidi idadi yake.

Kutokana na kuwapo idadi kubwa ya watu katika jiji la Mwanza, kwa siku wastani wa ng'ombe 200 huchinjwa katika jiji hili na katika halmashauri zake nane, ni wastani wa ng'ombe100, hata kufanya idadi yake kufikia ng'ombe 300 wanaochinjwa kwa mkoa mzima.

Pia, takwimu hizo zinasema idadi ya mifugo yote inayochinjwa mkoani hubadilika na kuongezeka siku za sikukuu hata kufikia wastani wa 500 kwa mkoa mzima, vilevile mbuzi na kondoo huchinjwa zaidi ya 100 kwa siku, lakini siku za sikukuu hufikia idadi ya 200.

Hivyo, wananchi watafaidika kupata nyama bora kupitia viwandani,kadhalika mifugo aina ya ng'ombe wa asili na kisasa wana faida kubwa ya kupata maziwa.

Kimsingi, serikali bado ina deni la kuhakikisha Mwanza kunajengwa kiwanda cha kutengeneza maziwa, badala ya kuwa na mifugo mingi isiyo na faida.

Tunahitaji wana Mwanza kuiunga mkono serikali kwa juhudi hizo ilizozifanya za kuwekeza viwanda vya nyama katika wilaya hizi, ili kuleta mabadiliko kiuchumi na mapinduzi makubwa ya kuongeza viwanda vingine vya aina hiyo katika mkoa wa Mwanza. Niseme, mifugo hiyo pia ina faida nyinginezo nyingi kama vile ngozi ambazo zinatakiwa kuwa na soko la uhakika, nadhani ingependeza sana kama serikali ingeweza kufikia lengo la kukifufua kiwanda cha ngozi cha zamani kilichokufa 'Mwanza Tanneries'.

Kiwanda hicho kilichopo Ilemela jijini hapa, kinaweza kurahisishia wafugaji na wananchi, pia wafanyabiashara wa zao hilo, kuuza bidhaa hizo kiwandani hapo.

Serikali nayo imekuwa ikitaja kukifufua, lakini inabaki na kitendawili hicho, kinachosubiri kuteguliwa kwa muda mrefu na huenda bado inajipanga au inaendelea kumsaka mwekezaji ambaye hajapatikana.

Kufufuliwa kiwanda hicho, naamini kutaleta mafanikio makubwa na mageuzi ya kiuchumi, ambayo yanatakiwa kuwa ya kisasa zaidi kwa ajili ya kutengeneza bidhaa za ngozi zitokanazo na mifugo yetu, katika kutengeneza mabegi, mikanda, viatu, pochi, waleti, mikoba na vitu vingine vingi.

Hapo ndiyo thamani ya zao la ngozi itaongezeka, soko litakuwepo la uhakika na wananchi hususani maskini, watafaidika kununua bidhaa zao za nyumbani kwa bei nafuu, badala ya kununua bidhaa zinazotoka nchi za nje.

Bidhaa nyingi zina gharama kubwa kuzinunua, pia wanazonunua wananchi maskini hazina ubora kudumu utumiaji wake,ikifahamika kuwa viwanda vya ngozi vilivyopo nchini viko mikoa ya Dar-es salaam, Morogoro na Moshi-Kilimanjaro.

Kama serikali itaweza kufufua kiwanda cha 'Mwanza Tanneries' itapunguza makali ya maisha ya wananchi, wanaotumia bidhaa zitokanazo na malighafi za ngozi zinazoagizwa kutoka nje ya nchi, kama vile Uganda, Kenya na Bara Ulaya au kwingineko, bei yake ikiwa kubwa na hawezi kuimudu mwananchi wa maisha ya chini, hivyo tunawapongeza serikali kufanya uwekezaji huo mkoani Mwanza.

HABARI KITAIFA

# Waziri Mabula aibua madudu, kusitisha ajira za mikataba sekta ardhi Dodoma

**Na Waandishi Wetu**

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, amesema hayuko tayari kuona madudu yanaendelea kutokana na vitendo vya ubadhirifu vinavyoendelea katika sekta ya ardhi Halmashauri ya Jiji la Dodoma.

Dk. Mabula alibainisha juzi kuwa kuna baadhi ya watendaji ambao wamekuwa wakirubuni wananchi kwa kuwadai hongo ili kuwapatia namba ya malipo (control number) na kuhoji kwa nini mwananchi anunue haki yake jambo ambalo ni kinyume cha maadili.

Waziri Mabula amebainisha hayo wakati wa ufunguzi wa kikao kazi kilichowakutanisha watendaji sekta ya ardhi na kampuni za upimaji katika Mkoa wa Dodoma.

Pia alionyesha kutoridhishwa kwake na huduma inayotolewa na vijana wenye ajira za kujitolea ambao alisema wamekuwa si weledi katika utoaji huduma za ardhi kwa wananchi na kuonya kuwa upungufu uliopo katika sekta hiyo jijini Dodoma unatokana na uwapo wa vijana hao ambao uchunguzi wa awali unaonyesha wanamiliki mali nyingi.

Kutokana na hali hiyo, Dk. Mabula alimwagiza Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma kufuta mikataba ya vijana hao ambao kwa kiasi kikubwa wana mmomonyoko wa maadili na wamekuwa chanzo cha migogoro ya ardhi.

Dk. Mabula alibainisha kuwa katika Halmashauri ya Jiji Dodoma, kuna vijana wengi wanaojitolea na hawalipwi na mamlaka hiyo lakini akahoji namna ambayo wamekuwa wakijipatia kipato bila kuwa na malipo kutoka taasisi yoyote.

Alionyesha kushangazwa na kitendo cha vijana hao kugomea kazi za muda mfupi katika mradi mpya wa Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi unaoendelea sehemu mbalimbali wakidai malipo ya Sh. 60,000 kwa siku hayatoshi.

Ni mazingira haya yanayomsukuma kiongozi huyo wa wizara kwenda mbali zaidi kumtaka Mkurugenzi wa Jiji Dodoma kuangalia upya vigezo vya ajira ya mkataba lakini pia kuwataka vijana hao kukabidhi ofisi na kama kuna miradi ambayo wanaisimamia waikabidhi haraka.

"Ni wapi vijana hawa wanapata fedha nyingi na wanamiliki vitu vyenye thamani zikiwamo magari na nyumba kama si kula rushwa? Wakiambiwa kuhusu kuajiriwa hawataki na hata tulijaribu kuwapa ajira ya muda katika mradi uliotayari kuwapa malipo ya Sh. 60,000 kwa siku hawakuwa tayari kwa madai kuwa malipo ni madogo," alisema.

Dk. Mabula amebaini kuwepo kwa watumishi wasio waadilifu wanaokiuka mpango kina uliopo na kudiriki kugawa viwanja katika eneo la makaburi na sehemu ya kingo za mto ili kuwagawia wananchi maeneo hatarishi akitaja tabia hiyo kama tamaa isiyofaa.

Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo Makazi, Mhandisi Anthony Sanga, aliwataka watendaji sekta ya ardhi nchini kuhakikisha wananchi wote wanaomiliki ardhi katika mkoa wa Dodoma wanasajiliwa katika mfumo wa ulipaji kodi ya pango la ardhi ili wapokee bili zao za malipo ya kodi kupitia simu zao za mkononi kama ilivyo katika bili za maji.

Pia aliwataka amewataka watendaji hao kuhakikisha wanamaliza migororo yote inayojitokeza katika sekta ya ardhi katika maeneo yote ambayo wanasimamia akiagiza kuwa hili pia ni maelekezo ya viongozi hivyo hawana budi kulifanyia kazi kwa umakini mkubwa.

# Mapacha wadaiwa kufa kwa kutumbukia shimoni

**Na Rose Jacob,** MWANZA

WATOTO mapacha wenye umri wa mwaka mmoja na miezi sita wamefariki dunia, baada ya kutumbukia kwenye shimo ambalo wazazi wao walilichimba kwa ajili ya kunyweshea mifugo.

Watoto hao ambao ni Kulwa Jimoku na Dotto Jimoku ambao wazazi wao ni Jimoku Rozalia (28) na Avelina Nkwaya (20), walitumbukia kwenye shimo hilo lililoko mita 30 kutoka iliko nyumba ya wazazi wao.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mwanza, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Wilbrod Mutafungwa, alisema tukio hilo lilitokea Aprili 23, mwaka huu, katika Kijiji cha Runele, wilayani Kwimba, wakati wazazi wakiendelea na shughuli za kilimo.

Aliwataja wazazi wa watoto hao kuwa ni Jimoku Rozalia (28) na Avelina Nkwaya (20).

Mutafungwa alisema chanzo cha vifo hivyo ni michezo ya watoto hao na uzembe wa wazazi kwa kutokuweka uangalizi kwao baada ya kuwaacha wenyewe na kwenda katika shughuli zao.

"Ninatoa wito kwa wazazi na walezi, kutimiza jukumu lao la msingi la kulea watoto na sio kuwaacha bila uangalizi wa mtu mzima, ili kuepuka madhara yanayoweza kujitokeza," alisema Kamanda Mutafungwa.

Alisema tayari miili hiyo imeshafanyiwa uchunguzi katika Hospitali ya Wilaya ya Kwimba na imekabidhiwa kwa familia kwa ajili ya maziko.


TRA

MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

Imethibitishwa na ISO 9001: 2015

## TAARIFA KWA UMMA

### WAFANYABIASHARA WAKAZI WAFANYAO BIASHARA MTANDAONI

**Dar es Salaam, 21 Aprili, 2023:**

Maendeleo ya teknolojia na matumizi ya vifaa vya kielektroniki yameleta mabadiliko makubwa katika uendeshaji wa biashara, ambapo, biashara (hususan ndogo na za kati) zinahama kutoka katika uendeshaji uliozoeleka wa kuwa na sehemu ya kudumu ya biashara kwenda katika kutumia njia za kidijitali (mtandaoni).

Kwa siku za hivi karibuni, kumekuwa na ongezeko kubwa la biashara za namna hii kufanyika kupitia mitandao mbalimbali ya kijamii. Mabadiliko haya yanatokana na utayari pamoja na utashi wa wafanyabiashara kwenda na wakati kwa kutumia teknolojia katika enzi hii ya kidijitali. Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) imebaini kuwa, baadhi ya wafanyabiashara za mitandao bila kufahamu au kwa makusudi, hawajajisajili kama Walipakodi kwa mujibu wa matakwa ya ***Kifungu cha 22 cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura. 438.***

Kwa kuzingatia maelezo hapo juu, TRA inapenda kuwakumbusha wafanyabishara (wakiwemo wale wa matangazo), kuhakikisha kuwa wanajisajili kwa mujibu wa Sheria za kodi. Mamlaka imeanza kufanya ufuatiliaji wa wafanyabiashara kwa njia ya mtandao ili kuwabaini wale wote ambao hawajajisajili na kuwachukulia hatua kwa mujibu wa sheria. Tafadhali, zingatia matakwa ya Sheria za Kodi ili kuepuka faini au adhabu zisizo za lazima.

Kwa taarifa zaidi, tafadhali tembelea ofisi yoyote ya TRA iliyo karibu nawe au wasiliana nasi kupitia; Simu za bure: **0800-750075/0800-780078/0800-110016** WhatsApp: **+255 7442-333 33** Barua pepe: **huduma@tra.go.tz** au **services@tra.go.tz** Mitandao ya Kijamii: ***Facebook: tratanzania*** *Twitter:* ***@tratanzania*** *Instagram:* ***@tratanzania***

*"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"*

Kidatah

A. J. Kidata

Kamishna Mkuu

173949

# DPP aagiza mapitio jalada la kesi uhujumu vigogo wa TPA

**Na Grace Gurisha**

MKURUGENZI wa Mashitaka (DPP), ametoa maelekezo kuwa jalada la kesi ya uhujumu uchumi inayomkabili aliyekuwa Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), Madeni Kipande (66) na wenzake wanne kuwa lipitiwe upya kabla ya kuendelea na hatua nyingine.

Aidha, inadaiwa kuwa DPP ametoa maelekezo hayo baada ya washtakiwa kuandika barua za malalamiko kuhusu mwenendo wa kesi hiyo.

Taarifa hiyo ilitolewa jana na Wakili wa Serikali, Mosie Kaima, mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Ramadhani Rugemarila wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam wakati kesi hiyo ilipoitwa kwa ajili ya kutajwa.

Kaima alidai kuwa kesi ililetwa kwa ajili ya kutajwa lakini wamepata maelekezo kutoka kwa DPP kuwa jalada la kesi hiyo lipitiwe upya kabla ya kuendelea na hatua nyingine.

"Tulikuwa kwenye hatua za mwisho za kuwasilisha taarifa Mahakama Kuu lakini wamepata maelekezo mapya kutoka kwa DPP. DPP alitoa maagizo haya baada ya washtakiwa kuandika barua za malalamiko kuhusu mwenendo wa kesi hiyo," alidai Kaima.

Baada ya taarifa hiyo, Hakimu Rugemalira aliahirisha kesi hiyo hadi Mei 18, 2023 kwa ajili ya kutajwa.

Mbali na Kipande, washtakiwa wengine ni Peter Gawile (58) aliyekuwa Mkurugenzi wa Rasilimali Watu na Utawala wa TPA, Casmily Lujegi (65) aliyekuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Ununuzi wa TPA, Mashaka Kisanta (59) aliyekuwa Mkurugenzi na Kilian Chale (51) Kaimu Mkurugenzi Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, wote wakazi wa Dar es Salaam.

Katika shitaka la kwanza Kipande na wenzake wanne, wanadaiwa kula njama ya kutenda kosa la kuisababishia TPA hasara ya Sh. bilioni 4.2 kati ya Oktoba Mosi, 2014 na Oktoba Mosi, 2020 jijini Dar es Salaam.

Inadaiwa kati ya Januari Mosi, 2015 hadi Februari 17, 2015 washtakiwa wakiwa maofisa wa TPA, walitumia madaraka yao vibaya kwa kutangaza zabuni namba AE/016/2014-15/CTB/G/39 kwa nia ya kujipatia Dola za Marekani 1,857,908.04 .

Pia inadaiwa Kati ya Oktoba Mosi 2014 na Oktoba Mosi, 2020 maeneo ya TPA na maeneo mengine ya Dar es Salaam, washtakiwa kwa makusudi walitangaza zabuni ya Enterprises Planning Resources (ERP).

Ilidaiwa walitangaza zabuni hiyo, bila kupata kibali cha bodi ya zabuni ya mamlaka hiyo na kushindwa kufuata kanuni za zabuni, hivyo kutoa malipo ya awali ya asilimia 40 bila idhini ya bodi, jambo lililoisababishia TPA hasara ya Dola za Marekani milioni 1.8 sawa na Sh. bilioni 4.2.

Julai 4, 2022 Kipande alisomewa mashtaka hayo matatu ya uhujumu uchumi akiwa kitandani katika Taasisi ya Tiba ya Mifupa na Mishipa ya Fahamu Muhimbili (MOI) baada ya kufanyiwa upasuaji wa mgongo.

# BAKWATA Bagamoyo yakemea ushoga

**Na Sabato Kasika,**
BAGAMOYO

BARAZA Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA) Bagamoyo mkoani Pwani, limekemea ushoga na kutaka taasisi zote zilizosajiliwa na baraza hilo zitakazobainika kujihusisha na uhamasishaji wa vitendo hivyo zifutwe.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Mwenyekiti wa BAKWATA Wilaya ya Bagamoyo. Abdul Sharif Zahoro, katika tamasha la kisomo cha Kurani wakati wa Sikukuu ya Idd kwenye viwanja vya Mwanakalenge.

Zahoro ambaye pia ni Mwenyekiti wa Taasisi ya Kiislam ya SHAKIBA ISLAMIC ya mjini hapa, iliyoandaa tamasha hilo, alisema Bagamoyo haitakuwa kichaka cha fedheha hiyo.

"Maadili haya hatutayakubali kabisa. Tunatahadharisha na tutalipambania hilo kwa nguvu zetu zote.

Taasisi zote zilizosajiliwa na baraza hili zitakazobainika kujihusisha na uhamasishaji wa vitendo hivyo zitafutwa," alisema Zahoro.

Shekhe Zahoro aliwaomba viongozi wa dini wote kutosita kukemea na kuonya jamii juu ya vitendo vya ushoga vinavyoendelea kufanywa na baadhi ya watu wasio na hofu ya Mwenyezi Mungu.

Mbunge wa Bagamoyo, Muharami Mkenge, aliwataka Waislamu na Watanzania kwa ujumla kumwombea Rais Samia Suluhu Hassan ili aendelee kuongoza nchi kwa amani na utulivu.

Alisem.a Rais ana majukumu mengi ya kulisimamia taifa, na kwamba ni muhimu kila Mtanzania kwa dini yake amuombee aweze kuliepusha na vikwazo mbalimbali, kwa kuwa maombi yana sehemu yake.

Taasisi ya SHAKIBA ISLAMIC iliandaa tamasha lililowakutanisha Waislamu kutoka wilayani humu na kupata fursa ya kufanya visomo vya kuruani na shughuli mbalimbali ikiwamo maandamano ya kupinga ushoga ili kutekeleza agizo la Mufti Mkuu wa Tanzania Shekhe Abubakari zuberi la kuandaa maandamano ya kupinga vitendo hivyo.



## FIRST HOUSING FINANCE (TANZANIA) LIMITED
## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

1st Housing

### IMETOLEWA CHINI YA KANUNI YA 7 NA YA 8 YA KANUNI ZA MABENKI NA TAASISI ZA FEDHA (UONESHAJI) YA MWAKA 2014

**WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31.03.2023**
(Kiasi kwa shilingi elfu)

| | | Robo Mwaka ya sasa 31st Mar. 2023 | Robo Mwaka iliyopita 31st Dec. 2022 |
|---|---|---|---|
| A. | MALI | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 11 | 1,532 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | - | - |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 3,655,981 | 3,601,363 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 4,942,240 | 6,695,407 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | - | - |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | - | - |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 21,493,405 | 19,561,504 |
| 12 | Mali Nyingine | 821,834 | 706,753 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | 1,622,000 | 1,622,000 |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 297,413 | 323,876 |
| 16 | **JUMLA YA MALI** | **32,832,883** | **32,512,435** |
| | | | |
| B. | B. DHIMA | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | - | - |
| 18 | Amana za Wateja | 1,134,403 | 911,787 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | - | - |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 603,121 | 1,054,642 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 363,237 | 41,070 |
| 27 | Dhima Nyingine | 338,405 | - |
| 28 | Madeni | 11,842,102 | 12,003,729 |
| 29 | **JUMLA YA DHIMA** | **14,281,268** | **14,011,228** |
| 30 | **MALI/(DHIMA) HALISI *(16 kutoa 29)*** | **18,551,615** | **18,501,207** |
| | | | |
| C. | FEDHA ZA WANAHISA | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 21,800,000 | 21,800,000 |
| 32 | Malipo juu ya bei ya hisa | - | - |
| 33 | Akiba ya Mtaji | 95,831 | - |
| 34 | Mapato Yaliyobakizwa | (3,491,108) | (3,678,678) |
| 35 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 50,409 | 284,054 |
| 36 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 96,483 | 95,831 |
| 37 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| 38 | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **18,551,615** | **18,501,207** |
| 39 | Dhima Zisizo Dhahiri | - | - |
| 40 | Mikopo Chechefu | 542,518 | 561,178 |
| 41 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 162,522 | 135,812 |
| 42 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| | | | |
| D. | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 56.50% | 56.91% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 2.50% | 2.85% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 1854.38% | 2160.30% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 65.46% | 60.17% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 90.92% | 91.84% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | 24.42% | 86.81% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 0.99% | 56.57% |

**TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31.03.2023** (Kiasi kwa shilingi elfu)

| | Maelezo | Robo ya Mwaka sasa 31st Mar. 2023 | Robo ya mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 31st Mar. 2022 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31st Mar. 2023 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 31st Mar. 2022 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 1,057,302 | 694,097 | 1,057,302 | 694,097 |
| 2 | Gharama za Riba | (325,660) | (69,467) | (325,660) | (69,467) |
| 3 | **Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **731,642** | **624,629** | **731,642** | **624,629** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (11,735) | (7,734) | (11,735) | (7,734) |
| 6 | **Mapato Yasiyo ya Riba:** | **78,326** | **85,774** | **78,326** | **85,774** |
| | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | (35) | 38 | (35) | 38 |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 78,362 | 53,350 | 78,362 | 53,350 |
| | 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| | 6.4 Mapato Mengine | - | 32,386 | - | 32,386 |
| 7 | **Gharama Zisizo za Riba:** | **(742,146)** | **(647,147)** | **(742,146)** | **(647,147)** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (391,817) | (326,130) | (391,817) | (326,130) |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | - | - | - | - |
| | 7.3 Gharama Nyingine | (350,329) | (321,017) | (350,329) | (321,017) |
| 8 | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **56,088** | **55,523** | **56,088** | **55,523** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | (5,678) | (3,899) | (5,678) | (3,899) |
| 10 | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **50,409** | **51,623** | **50,409** | **51,623** |
| 11 | Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha) | - | - | - | - |
| 12 | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa robo ya mwaka /mwaka** | **50,409** | **51,623** | **50,409** | **51,623** |
| | | | | | |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 24 | 20 | 24 | 20 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | 0.23 | 0.24 | 0.23 | 0.24 |
| 15 | Idadi ya Matawi | 1 | 1 | 1 | 1 |
| | | | | | |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (i) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 0.15% | 0.23% | 0.15% | 0.23% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 0.27% | 0.28% | 0.27% | 0.28% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 91.63% | 91.10% | 91.63% | 91.10% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 2.45% | 3.13% | 2.45% | 3.13% |

**TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31.03.2023** (Kiasi kwa shilingi elfu)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo (Bainisha) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Robo ya mwaka ya sasa (31.03.2023)** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa robo ya mwaka (01.01.2023)** | **21,800,000** | **-** | **(3,456,954)** | **62,328** | **-** | **95,831** | **18,501,205** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 50,409 | - | - | - | 50,409 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | (34,155) | 34,155 | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa robo ya mwaka (31.03.2023)** | **21,800,000** | **-** | **(3,440,699)** | **96,483** | **-** | **95,831** | **18,551,615** |
| | | | | | | | |
| **Robo ya mwaka iliyopita (31.12.2022)** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka (01.10.2022)** | **21,800,000** | **-** | **(3,590,252)** | **12,974** | **-** | **95,831** | **18,318,554** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 182,652 | - | - | - | 182,652 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | (49,354) | 49,354 | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa robo ya mwaka (31.12.2022)** | **21,800,000** | **-** | **(3,456,954)** | **62,328** | **-** | **95,831** | **18,501,207** |

**TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31.03.2023** (Kiasi kwa shilingi elfu)

| | | Robo ya Mwaka sasa 31st Mar. 2023 | Robo ya Mwaka iliyopita 31st Dec. 2022 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31st Mar. 2023 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 31st Mar. 2022 |
|---|---|---|---|---|---|
| I: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | **56,088** | **191,438** | **56,088** | **55,523** |
| | **Marekebisho kwa Ajili ya:** | - | - | - | - |
| | - Hasara Katika Mali | (492,333) | 23,378 | (492,333) | 87,616 |
| | - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (2,051,095) | (1,152,760) | (2,051,095) | (891,093) |
| | - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 222,616 | 170,099 | 222,616 | (70,014) |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 203,372 | (136,378) | 203,372 | 294,316 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (109,403) | 63,784 | (109,403) | (166,469) |
| | - Kodi iliyolipwa | (5,678) | (18,838) | (5,678) | (3,899) |
| | - Mengineyo | 50,443 | 24,008 | 50,443 | 52,923 |
| | ***Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji*** | ***(2,125,990)*** | ***(835,269)*** | ***(2,125,990)*** | ***(641,099)*** |
| II: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | |
| | Gawio Lililopokewa | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | 637,991 | (2,207) | 637,991 | (16,988) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | (54,618) | 51,758 | (54,618) | (51,126) |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| | ***Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji*** | ***583,374*** | ***49,551*** | ***583,374*** | ***(68,113)*** |
| III: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu kwenda CRDB | (161,627) | 1,753 | (161,627) | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| | Deni jipya kutoka CRDB Bank | - | - | - | 2,839,173 |
| | Mengineyo (bainisha) | (50,445) | - | (50,445) | (49,702) |
| | ***Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha*** | ***(212,072)*** | ***1,753*** | ***(212,072)*** | ***2,789,471*** |
| | | | | | |
| IV: | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | | |
| | **Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha** | **(1,754,689)** | **(783,964)** | **(1,754,689)** | **2,080,259** |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 6,696,939 | 7,490,961 | 6,696,939 | 945,786 |
| | Badiliko Halisi Katika Mikopo ya mabenki | - | (10,057) | - | (3,221) |
| | **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka** | **4,942,251** | **6,696,939** | **4,942,251** | **3,022,824** |

**MINIMUM DISCLOSURES OF CHARGES AND FEES FOR THE YEAR 2023**

| S/No | ITEMS | CHARGES/FEES |
|---|---|---|
| 1 | Prime Lending Rate (PLR) | 16% p.a. |
| 2 | Maximum spread above PLR | 4% p.a. |
| 3 | Application Fee (Non-refundable) | TZS 200,000/- |
| 4 | Processing Fee | 1.5 % of the loan value |
| 5 | Facility Fee | 1.5 % of the loan value |
| 6 | Valuation Fee | Paid by the client as per the invoice |
| 7 | Legal Fee | Paid by the client to FHF account and FHF will pay law firm |
| 8 | Early Repayment | 5% of the amount to be prepaid |
| 9 | Annual Review Fee | NIL |
| 10 | Cheque returned Unpaid (Outward & Inward) | TZS 50,000/- |
| 11 | Loan Statement | TZS 20,000/- |

Katika kuanda taarifa hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilizile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita (kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya/mwaka wa sasa, mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8).

| *Jina na Cheo :* | *Saini* | | *Tarehe* |
|---|---|---|---|
| Sasa M. Chonza **(Ofisa Mtendaji Mkuu)** | (Imesainiwa) | ............................. | **25.04.2023** |
| Amulike Kamwela **(Mkuu wa Fedha)** | (Imesainiwa) | ............................. | **25.04.2023** |
| Isambo Binde **(Mkaguzi Mkuu wa Ndani)** | (Imesainiwa) | ............................. | **25.04.2023** |

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi).

| *Jina:* | *Saini* | | *Tarehe* |
|---|---|---|---|
| Conrad D'souza **Mwenyekiti** | (Imesainiwa) | ............................. | **25.04.2023** |
| Vinod Rustagi **Mkurugenzi** | (Imesainiwa) | ............................. | **25.04.2023** |




173951





# Jela miaka 60 kwa kumbaka mwanafunzi

**Na Godfrey Mushi, SIHA**

MKAZI wa Kijiji cha Matadi, Siha mkoani Kilimanjaro, Abeid Kingazi (36), amehukumiwa kutumikia kifungo cha miaka 60 jela baada ya kutiwa hatiani kwa kosa la kumbaka na kumpa ujauzito mwanafunzi wa shule ya msingi.

Kingazi, alihukumiwa kutumikia adhabu hiyo juzi na Mahakama ya Wilaya ya Siha.

Akisoma hukumu hiyo, Hakimu Mkazi Mfawidhi, Jasmin Abdul, alisema mahakama imejiridhisha kwamba mshtakiwa alitenda kosa hilo kwa makusudi huku akijua kufanya hivyo ni kosa kisheria.

Kwa mujibu wa hakimu huyo, upande wa mashtaka katika kesi hiyo umeijenga kesi hiyo na kutoacha shaka yoyote, hivyo mahakama imeamua kumpa kumshtakiwa adhabu hiyo ili kukomesha matukio hayo ya ukatili wa kingono. Katika kesi hiyo, mahakama ilisikiliza ushahidi wa watu wanne wa upande wa mashtaka ambao ni pamoja na mwathirika wa tukio hilo na daktari aliyefanya uchunguzi wa kitabibu.

Kosa la kwanza ambalo mshtakiwa huyo ametiwa nalo hatiani na kupewa adhabu ya miaka 30 jela ni la kubaka ambalo ni kinyume cha kifungu 130 (1) (2) (e) na 131 cha Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16 ya Sheria iliyofanyiwa marejeo mwaka 2002.

Kosa la pili alilopewa adhanu ni la kumpa ujauzito mwanafunzi ni kinyume cha kifungu 60 A (3) cha Sheria ya Elimu, Sura ya 353; ambalo nalo adhabu yake ni kifungo cha miaka 30 jela.

Awali, katika hati ya mashtaka iliyosomwa mahakamani humo na Mwendesha Mashtaka wa Serikali, David Chishimba, mshtakiwa anadaiwa kutenda makosa hayo tarehe tofauti tofauti, mwaka jana katika kijiji cha Matadi.

Pia ilidaiwa kuwa kabla ya kutekekeleza tukio hilo, mshtakiwa alimdanganyi mwanafunzi huyo ambaye ni shemeji yake, amwingilie kingono ili apone ugonjwa uliokuwa unamsumbua wa kutoka damu sehemu za siri na puani. Aidha, mwendesha mashtaka katika kesi hiyo, alidai kuwa mshtakiwa aliamua kwenda kwa waganga wa kienyeji ili kupata tiba, na aliporudi alimwambia mwanafunnzi huyo kwamba ili apone ni lazima amuingilie kimwili mara tatu.

## Serikali yataka kuundwa mabaraza ulinzi watoto

**Na Allan Isack,** ARUMERU

SERIKALI imeagiza kuundwa mara moja kwa mabaraza na madawati ya ulinzi na usalama kwa watoto katika Halmashauri ya Meru, mkoani Arusha ili kuwaepusha dhidi ya matukio ya ukatili yanayoendelea kuchipua kila uchao.

Aidha, madawati na mabaraza hayo yanalenga kuimarisha utekelezaji wa haki, ulinzi na usalama wa watoto, kwa kuwa ni lazima waishi katika mazingiza ambayo ni salama popote watakapokuwa.

Jana, Mratibu wa Mpango wa Shule Salama kutoka Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Hilda Mgomapayo, alielekeza uundwaji huo kufanywa na maofisa maendeleo ya jamii, ustawi wa jamii na waratibu wa elimu kata.

"Maelekezo ya serikali ni haya. Mosi, mabaraza yaanzishwe kuanzia ngazi za vijiji, mitaa, kata hadi wilaya ili kuboresha na kuweka mazingira salama kwa watoto wakiwa ndani na nje ya shule.

"Serikali katika kuimarisha upatikanaji wa haki na usalama wa mtoto, inatekeleza Mradi wa Kuimarisha Ufundishaji na Ujifunzaji kwa Shule za Awali na Msingi Tanzania (BOOST)."

Aidha, alisema katika hatua ya kuboresha na kuweka vizuri mazingira ya kujifunzia kwa wanafunzi, pia serikali inatekeleza Mradi wa Uboreshaji Elimu ya Sekondari (SEQUIP), kwa ajili ya kuwawezesha wanafunzi kukamilisha mzunguko wa elimu yao.

Katika hatua nyingine, amelipongeza Shirika la SOS Children's Village, kwa namna wanavyoshirikiana na serikali kuhakikisha watoto wanalindwa dhidi ya vitendo vya ukatili wa kijinsia.

Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Halmashauri ya Meru, Flora Msilu, akizungumza katika hafla ya utoaji mafunzo ya siku tatu kwa mabaraza na madawati hayo, amelishukuru Shirika la SOS Children's Village kwa kuisaidia serikali kutoa elimu hiyo.




Baadhi ya wauguzi na wataalamu wengine wa afya mkoani Manyara, wakiwa kwenye maandamano wakati wa uzinduzi wa Wiki ya Chanjo Duniani, katika Uwanja wa Kwaraa, mjini Babati juzi. **PICHA: JALIWASON JASSON**

# RC asema dawa ya magendo 'imeiva'

**Na Hamida Kamchalla,**

TANGA

MKUU wa Mkoa wa Tanga, Waziri Kindamba, amesema serikali imepata 'dawa' ya biashara ya magendo katika mwambao wa Bahari ya Hindi, ambako wafanyabiashara wakubwa wamekuwa wakikwepa mtego wa maofisa mapato wanaofuatilia nyendo zao.

Akizungumza jana katika viunga vya bandari ya Tanga, wakati wa hafla ya kukabidhi boti ya doria, Kindamba alisema boti hiyo ni mahususi kwa ajili ya kuzuia, kupambana na ujangili na magendo yanayofanyika katika eneo hilo.


"Nawatahadharisha tu ni bora mlipe kodi halali, kwa sababu mnaojihusisha na upitishaji wa magendo tutawafuata kokote watakapopita. Boti hii pia itatumika kupambana na uingizaji na usambazaji wa dawa za kulevya kuingia mkoa wa Tanga, kwa sababu mara nyingi sehemu za pwani zimekuwa njia kuu za kupitishia dawa hizo.

"Na kwa muktadha huo, ni lazima wananchi wa Tanga wajue kwamba kuingiza bidhaa nchini kwa njia ya magendo ni ukwepaji wa kodi. Hakuna sababu ya kufanya magendo, watoaji wa huduma ambao ni Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) wapo na wanatoa huduma nzuri bila ubabaishaji," alisema.

Kutokana na ujio wa boti hiyo, mkuu huyo wa mkoa alisema kwa sasa hakuna namna nyingine zaidi ya wafanyabiashara kupitisha mizigo yao kwa njia halali.

Kabla ya makabidhiano hayo, Naibu Kamishna wa Ushuru na Forodha wa TRA, Godfrey Kitundu, alisema boti hiyo ni moja ya boti tatu ambazo zilinunuliwa katika bajeti mwaka 2021/22.

Kwa mujibu wa Kitundu, kila boti imegharimu zaidi ya Sh. milioni 529.





# PASS yajizatiti kukomboa wakulima

**Na Titus Mwombeki,** KAGERA

SHIRIKA lisilo la kiserikali la PASS Trust linalojihusisha na huduma ya udhamini kwa wakulima na wafugaji, imejipanga kuendelea kulisaidia kundi hilo, ili kuhakikisha wanapata mikopo katika taasisi za kifedha kwa lengo la kuboresha shughuli zao za kilimo na ufugaji.

Akizungumza katika uzinduzi wa Kampeni ya Kijanisha Maisha, Mkurugenzi wa Biashara wa shirika hilo, Adam Kamanda, alisema katika kipindi cha mwaka jana, wakulima kupitia taasisi 66 zisizo za kiserikali mkoani humo, walidhaminiwa na shirika hilo na kukopeshwa na benki mbalimbali Sh. bilioni 31.

Kamanda alisema kuwa kampuni hiyo huwasaidia wakulima wenye lengo ya kupanua wigo wa kilimo bora ambacho akiathiri mazingira ili kuweza kujipatia kipato pamoja na kutunza mazingira.

Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Albert Chalamila, alilipongeza shirika hilo kwa kuwasaidia wakulima pamoja na wafugaji na kuwataka viongozi wake kusaidia pia, upatikanaji wa soko la mazao yao baada ya kuvuna.

Mkurugenzi wa shirika la Kahama Fresh, Joswam Ntangeki, ambaye pia ni mwekezaji katika sekta ya kilimo mkoani Kagera alisema Shirika la Pass Trust limekuwa msaada kwa wakulima hasa katika kuwadhamini.

# Wachimbaji waonywa uharibifu mazingira

**Na Marco Maduhu,** GEITA

WACHIMBAJI wadogo wa dhahabu mkoani Geita, wameonywa tabia ya kuchimba na kutelekeza mashimo hovyo baada ya kumaliza shughuli zao, hali inayohatarisha uhifadhi wa mazingira katika eneo husika.

Badala yake wametakiwa kupanda miti katika maeneo hayo ili kuhifadhi mazingira.

Mkuu wa Wilaya ya Geita, Cornel Magembe, alitoa onyo hilo juzi na kusema kwamba asilimia 70 ya wakazi mkoani hapa hujishughulisha na uchimbaji mdogo wa madini, na kuwataka kuangalia suala la utunzaji wa mazingira.

Alisema suala la utunzaji wa mazingira lipo kisheria na siyo takwa la mtu bali ni kwa faida ya vizazi vijavyo. "Wakimaliza kuchimba wanaacha mashimo wazi na kuhatarisha hali ya mazingira katika machimbo husika, hali hii ikiendelea hivi, tutatengeneza jangwa," alisema.

Kaimu Ofisa Madini Mkoa wa Geita, Mhandisi Martin Shija, aliwataka wachimbaji wadogo kutekeleza mpango wa utunzaji mazingira kwa ajili ya maendeleo endelevu na vizazi vijavyo.

Alisema sheria iko wazi kwa wale ambao hawatekelezi mpango huo, kwamba wanaweza kunyang'anywa leseni zao.

Meneja wa Mgodi wa STAMICO Gold Mining Operative Society Ltd ulioko Nyarugusu wilayani Geita, Hoja Shikome alisema wachimbaji wadogo wamekuwa wakichimba kwa kubahatisha kutokana na kutokuwa na vifaa vya kisasa vya kubaini maeneo yenye madini.

"Hali hii inahatarisha mazingira kwani, bila kupima na kujua maeneo yenye madini, huwafanya wachimbaji hawa kukata hovyo miti wakitafuta maeneo yenye madini, hivyo kuacha maeneo hayo bila kurudishia miti iliyokatwa," alisema.

Alisema wakati wanafika kwenye machimbo ya Nyarugusu kwenye mgodi huo wa Stamico na kuanza shughuli za uchimbaji, walikuta mashimo mengi ambayo yameachwa na wachimbaji wadogo na kuanza kuyafukia wakati wakiendelea na uchimbaji madini eneo jingine.

Ofisa Mazingira mkoani hapa, Tito Mlelwa, aliwataka wachimbaji wadogo wa madini ya dhahabu, kuiga mfano wa mchimbaji mwenzao, Geita Resources katika machimbo ya Nyamatagata, ambaye akimaliza kuchimba madini hufukia eneo husika na kupanda miti.

Ofisa Miradi kutoka timu ya Wanasheria Watetezi wa Mazingira kwa Vitendo (LEAT), Clay Mwaifwani, alisema wamekuwa wakihamasisha suala la utunzaji wa mazingira kwenye machimbo ili kuwapo na uchimbaji salama usiyoathiri mazingira.



Baadhi ya wakazi wa kitongoji cha Nyamongo, wilayani Tarime, wakipatiwa huduma za afya wakati wa maadhimisho ya Siku ya Malaria Duniani, katika viwanja vya Shule ya Sekondari ya Nyamongo, kwa ufadhili wa mgodi wa Barrick North Mara juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wasisitizwa umuhimu wa chanjo kwa watoto

**Na Mwandishi Wetu**

VIONGOZI mbalimbali wameendelea kuwasisitiza wazazi na walezi kuhusu umuhimu wa chanjo kwa watoto pamoja na wajawazito, kwa lengo la kuimarisha na kulinda afya za watoto.

Mkuu wa Wilaya ya Geita, Cornel Magembe, alisema juzi katika maadhimisho ya Wiki ya Chanjo yaliyofanyika katika Kituo cha Afya cha Nyankumbu, Halmashauri ya Mji Geita mkoani hapa, kuwa chanjo hiyo ni muhimu kwa wajawazito na watoto. Kiongozi huyo akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa huo, alisema ili kuhakikisha wanakuwa na watoto wenye akili na afya njema, ni vyema wazazi na walezi kuzingatia maelekezo ya madaktari kuhusu utolewaji wa chanjo. Pia alisema kuna umuhimu wa wanaume kuchukua jukumu la kuwahimiza wake zao kwenda kliniki na kufuata utaratibu wanaopewa na wahudumu wa afya ili kuokoa taifa na maradhi yenye kinga, ikiwa ni pamoja na surua rubella na polio.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Geita, Dk. Omari Sukari, alisema katika kipindi cha mwaka 2022, walifanikiwa kufikia lengo la kutoa chanjo hizo kwa asilimia 100, huku wakitarajia kuwafikia watoto zaidi ya 23,000 wenye umri wa miaka sifuri hadi mitano.

Kwa upande wa Mwanza, Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana, Amina Makilagi, alisema chanjo hizo zimeokoa maisha ya watanzania wengi, lakini kuna baadhi ya watoto na wasichana hawajapata na lengo, ni kuhakikisha kila anayestahili aweze kupata.

Alisema wataendelea kuweka bidii katika utekelezaji wake pamoja na kutoa elimu kwa jamii kuhusu umuhimu wake ili kuwafikia walengwa wote.

Mganga Mkuu wa Jiji la Mwanza, Dk. Sebastian Pima, alisema mwaka 2022 wilaya ya Nyamagana, walengwa wa chanjo ambao ni watoto chini ya miaka mitano walikuwa 23,004 ambapo kati ya hao, waliopata chanjo ya tatu ( Pentavalent3) ni 22,645 sawa na asilimia 98.

**Imeandaliwa na Alphonce Kabilondo (GEITA) na Neema Emmanuel (MWANZA)**

ama
ALHAMISI APRILI 27, 2023
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 12

**MSD inavyokuwa mkombozi Hospitali Rufani mkoa Dodoma, inazaliwa upya**



Ukurasa 13

Kamanda Mohamed wa TFS Kanda ya Ziwa asimulia ndani, nje vita vyao kuokoa misitu



Ukurasa 14

**SBL yawajibikia jamii kupitia 'Lengo la Sita SDG' maji imfikie mama Handeni**

AFYA

# Chanjo aliyozindua Rais yajibu makubwa kimataifa, WHO ikimwaga pongezi kuu

**Na Yasmine Protace**

NADHARIA ya tiba kuhusu chanjo inajulikana na kongwe, ikiwa na nafasi kubwa ya kinga kiafya mtu asiugue. Chanjo kwa jumla, inatajwa kuzuia vifo milioni mbili kila mwaka duniani.

Pale ulipoibuka ugonjwa wa Uviko 19 duniani, nao ukaleta mapya, suala la kinga kupitia chanjo, ikiwa ni zao la watafiti walioumiza vichwa haraka, ukaibua mbinu mpya ya kivita dhidi ya maradhi hayo.

Nchini, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, miezi kadhaa akiwa madarakani mwaka 2021, akishikia vibwebwe baada ya kupatikana misaada ya dawa za chanjo hizo, akaamua kuhamasisha kampeni ya chanjo na uzinduzi wake akaonyesha hadharani, yeye akiwa wa kwanza na watendaji wakuu kiserikali, wakiwamo mawaziri na wakuu wa vyombo va ulinzi na usalama nchini.

Hadi sasa hatua imefika pazuri, kwamba chanjo inapatikana kila mtaa ikiwamo katika zahanati za mitaani binafsi na za serikali, kasi ya Uviko 19 nayo imepungua mno, hata uvaaji barakoa kitaifa unapatikana kwa nadra. Kwa kifupi, kampeni za Rais Dk. Samia kuzindua chanjo imetekelezwa kwa ufanisi na mwitikio ni wa ngazi ya juu.

Tangu kampeni hiyo kuzinduliwa, ripti mbalimbali zakiimataofa zimekuwa zikitokewea kusifu Tanzania kwamba ni kati ya nchi zilizoonyeshja ufanisi mkubwa katika kufanikisha Chanjo ya Uviko 19, barani Afrika salamu zikitumwa hata na Shirika la Afya Duniani (WHO), inayoiwerkia katika. nchi tano bora batrami humo.



Siku Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, alipozindua kampeni ya chanjo kitaifa dhidi ya Uviko 19, mwaka 2021. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

Pia, ni siku chache zilizopita, Mwakilishi Mkazi wa WHO nchini, Dk. Boniface Makelemo, ameipongezaa serikali kwa hatua thabiti zinazochukuliwa kupunguza athari za magonjwa yanayozuilika kwa chanjo.

Anasema, WHO na washirika wao wote wa chanjo wanaunga mkono juhudi za serikali na kujitolea rasilimali za watu na fedha, kuinua kiwango cha chanjo kwa watu wote wanaostahili chanjo kwa rika zote.

Kuhusu chanjo ya UVIKO-19, Dk.Makelemo anasema Tanzania imepiga hatua kubwa katika utoaji wa chanjo hiyo, asilimia 52 ya wananchi wamepata chanjo.

Taarifa ya ofisi ya WHO Tanzania, jijini Dar es Salaam, inasema wakati utoaji wa chanjo dhidi ya UVIKO-19 ukiingia katika hatua ya kuunganishwa na huduma za kawaida, Tanzania imekuwa nchi inayofanya vizuri zaidi kati ya nchi 34 za Afrika zilizokuwa na idadi ya chini ya asilimia 10 ya watu waliolengwa kupata chanjo hiyo hadi Januari 2022.

WHO, Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF), na Muungano wa Chanjo (Gavi), walizindua Ushirikiano wa Kutoa Chanjo dhidi ya UVIKO-19 (CoVDP) Januari 2022 ili kuwezesha chanjo hiyo kutolewa kwa haraka na kulinda jamii zilizo katika mazingira hatarishi kwa kuchanja watu wake.

Hadi sasa serikiali inaeleza imeweka mikakati ya kuhakikisha huduma za afya husussani za chanjo zinaendelea kuboreshwa, ikiwemo kununua dawa za chanjo unafanyika kwa wakati, ili kuwa na rasilimali za kutosha muda wote na kuongeza majokofu ya kisasa inayoimarisha mnyororo baridi,i kuhakikisha kuwa chanjo zinazotolewa kuwa katika ubora.




Dawa za chanjo aina ya Janssen zilizowasilishwa nchini.

**INAENDELEA UK.14**

AFYA

# MSD inavyokuwa mkombozi Hospitali Rufani mkoa Dodoma, inazaliwa upya



Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani Mkoa wa Dodoma, Dk.Ibenzi Ernest, akionyesha moja ya mashine zilizopelekwa na MSD katika Hospitali ya Rufani mkoa wa Dodoma. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

**Na Elizabeth Zaya**

MGANGA Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani mkoa wa Dodoma, Dk.Ibenzi Ernest, anaitaja Bohari Kuu ya Dawa (MSD), ndio taasisi inayowajibika kuiwezesha upatikanaji wa vifaa vipya na vya kisasa.

Anasema miaka ya nyuma kidogo, hospitali hiyo haikuwa na uwezo wa kufanya vipimo vya aina yoyote kwa wagonjwa wake, na hivyo walilazimika kuwapeleka wagonjwa wao Morogoro au Hospitali ya Taifa Muhimbili.

"Kwa sasa mambo yamebadilika, ile historia mbaya ya Hospitali ya Rufaa ya Dodoma imefutika, kwa sasa tuna vifaa vizuri vya kisasa ambavyo hata katika hospitali nyingine hawana, na kazi hii nzuri imefanywa na MSD,"anasema Dk.Ernest.

"Mashine zote za kisasa za kupimia zilizopo katika hospitali ya rufaa ya mkoa wa Dodoma tumepata MSD, zamani vipimo tulikuwa tunalazimika kuvituma mpaka Dar es Salaam ndio vikapimwe halafu turudishiwe tena, lakini kwa sasa kila kitu tunafanya sisi wenyewe baada ya kupata vifaa hivi.

"Kama ni maboresho, kati ya asilimia 10, sisi tumefikia asilimia 9.8 ukilinganisha na kule tulikotoka, yaani tumebadilika pakubwa sana, ilikuwa ni aibu mwanzoni, mgonjwa alikuwa akija hapa kumpima unapima wingi wa damu tu.

Anasema kabla ya kupata vifaa hivyo, walikuwa na uwezo kuhudumia wagonjwa watatu tu waliozidiwa kwenye chumba cha dharura, kwa sasa baada ya kupata vifaa kutoka MSD wanahudumia wagonjwa waliozidiwa 36 na kila mgonjwa anakuwa na kifaa chake.

> **Maghala yamejengwa kwa kufuata vigezo vinavyokubalika vya ubora ili kuhifadhi bidhaa za afya kwa kufuata miongozo ya watengenezaji. Bidhaa zote zinapokelewa, zinatunzwa na kutolewa ghalani kwa kutumia mfumo.**

"Sasa hivi ukienda maabara unashangaa tu, maana vifaa vilivyopo kwa sasa hatujawahi kuwa navyo. Miaka ya 2014 kurudi nyuma wagonjwa wengi walikuwa wakija hapa hospitalini na kuangalia mazingira walikuwa hawakubali kutibiwa, lakini leo tunazungumza historia mpya.

"Tuna mashine za kisasa ambazo ukifanya vipimo, ndani ya dakika moja tu zimeshatoa majibu kwa sababu zimeunganishwa na intaneti, majibu huwa yanaenda moja kwa moja kwa daktari. Zamani kabla ya kupata mashine hizi, tulikuwa tunapiga picha kwenye mashine za kizamani halafu tunazibeba kwenda kuzianika wakati mwingine hadi saa tatu ndio majibu yaanze kusoma.

"Kwa hiyo imerahisisha sana majibu yanatoka haraka, yanafika kwa daktari haraka, lakini pia imepunguza gharama na vitu vingine kama hivyo. Zamani tulikuwa ukipiga 'exlay' mgonjwa mmoja mpaka ukae tena dakika 15 ndio umpige mwingine, lakini mashine za sasa hivi ni unapadisha mgonjwa mmoja na unamshusha hapo hapo na unampandisha mwingine, kwa hiyo ndani ya saa moja unaweza kupiga hata 'x-ray' 100."

Dk. Ernest anadems, miaka ya nyuma mashine zilikuwa mbili tu kwa mkoa wa Dodoma, moja katika hospitali ya Dodoma na nyingine Hospitali ya Mirembe.

"Kwa hiyo ikiharibika, wagonjwa tulikuwa tunawaambia wakapige Dar es Salaam au Morogoro. Tunashukuru sana uwekezaji ambao umefanywa na Rais Samia Suluhu Hassan, hospitali yetu inavyoonekana kwa sasa si kama ilivyokuwa zamani, tulikuwa na changamoto kubwa ya upatikanaji wa dawa na vifaa tiba, lakini kwa sasa tunapata dawa nyingi na vifaa tiba vya kutosha kutoka MSD,"anasema.

"Zamani ulikuwa ukifika hapa ukiangalia mazingira unawaza hivi nitapona kweli, lakini kwa sasa ukifika unaona tayari una nafasi kubwa ya kupona. Hivi vifaa tiba vilivyopo hapa kwa sasa zamani tulikuwa tunaviona tukienda kwenye hospitali za wenzetu."

Anasema upatikanaji wa dawa kwa sasa katika hospitali hiyo ni asilimia 96 kutoka asilimia 40 ya mwanzo.

Mkuu wa kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano MSD, Etty Kusiluka, anasema asilimia 95 ya vitu vilivyopo katika hospitali hiyo vinatoka MSD ukitoa meza, kompyuta na viti wanavyotumia wafanyakazi.

"Lakini kuanzia vitu wanavyovaa, yaani vitambaa vya sare zao za kazi, mashine, vitanda, magodoro, kadi za wagonjwa, kalamu, dawa, vifaa vya maabara, na kila kitu kilichopo katika hospitali hii kimetoka MSD,"anasema Kusiluka.

Mkurugenzi Mkuu wa MSD, Tukae Mavere anasema Bohari hiyo hufanya usambazaji wa bidhaa za afya hadi mlangoni mwa vituo vya afya kila baada ya miezi miwili mara sita kwa mwaka na kuvifikia vituo vya kutolea huduma za afya vya ngazi zote.

"Usambazaji wa bidhaa za afya unafanyika kwa kutumia magari 185 ambapo bidhaa hupakiwa kwa mujibu wa mahitaji ya wateja na hupokelewa kwa kutumia mfumo wa kielektroniki unaotunza takwimu za upokeaji (Proof of Delivery).

Kuhusu maboresho wanayofanya, Mavere anasema ili kuendana na maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan, MSD inafanya mapitio ya mnyororo wa ugavi ili kuimarisha ununuzi wenye tija, kuepuka upotevu na kupata bidhaa kwa bei nzuri.

Kufunga mashine zaidi katika maabara na usambazaji wa vitendanishi ili kusogeza huduma kwa wananchi, kupunguza gharama za uchunguzi, na kuongeza upatikanaji wa huduma kwenye vituo.

Pia, anasema wamejipanga zaidi kwa usimamizi na kuimarisha mifumo ya usimamizi wa vihatarishi, kuwezesha kazi zote za mnyororo wa ugavi kufanyika kijiditali.

Nyingine anasema ni kuimarisha usimamizi wa watumishi kwa kuboresha mifumo ya upimaji utendaji kwa kutumia mifumo ya kidigitali, kuboresha usimamizi wa shughuli za taasisi kupitia ofisi ya kimkakati.

Kuhusu uboreshaji wa miundombinu ya kuhifadhi bidhaa za afya, Mavere anasema MSD imeendelea kuwekeza pia katika eneo hilo kwa kuhakikisha inakuwa na maghara ya kutosha kwa ajili ya kuhifadhia.

Anasema wanayo maghala ya kuhifadhia katika maeneo mbalimbali ya nchi ikiwamo yenye ukubwa wa mita za mraba 69,758.57, ambayo mengine huwezesha kuhifadhi bidhaa toshelevu za miezi tisa.

"Maghala yamejengwa kwa kufuata vigezo vinavyokubalika vya ubora ili kuhifadhi bidhaa za afya kwa kufuata miongozo ya watengenezaji. Bidhaa zote zinapokelewa, zinatunzwa na kutolewa ghalani kwa kutumia mfumo,"anasema.

Kuhusu mkakati wa MSD katika kuendana na ukuaji wa sekta ya afya nchini, Mavere anasema ni kuhakikisha wananunua bidhaa kutoka kwa wazalishaji nchini ili kupunguza muda wa uagizaji na kuwajengea uwezo wazalishaji, kufanya ununuzi moja kwa moja kutoka kwa wazalishaji wa nje kwa bidhaa zisizokuwapo nchini ili kupunguza bei na kupata bidhaa kwa wingi.

Jinginme anasema ni kutumia mifumo ya ununuzi ya kidigitali na kuwa na mikataba ya muda mrefu, kukamilisha uanzishwaji wa kampuni tanzu itakayosimamia uendeshaji wa viwanda, kuendelea kuimarisha upatikanaji wa bidhaa za afya ashiria kufikia asilimia 90, kufuatia matumizi ya bidhaa za afya, kupunguza upotevu na kuboresha upatikanaji.

MAZINGIRA

# Kamanda Mohamed wa TFS Kanda ya Ziwa asimulia ndani, nje vita vyao kuokoa misitu

## • Asali hawako nayo mbali... majangili nao 'wanaipata'

**Na Anthony Gervas,** MWANZA

TFS ni Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania, ambayo katika Kanda ya Ziwa iko katika juhudi na mipango mikakati yake, kupigania rasilimali za misitu na nyuki, pia kutunza mazingira.

Bakari Mohamed, ni Kamanda wa TFS Kanda ya Ziwa, pia akiwajibika kuwa Mhifadhi Mkuu wa Misitu, anaifafanulia Nipashe kuwa hadi sasa wana mpango unaoipa majukumu makubwa, ambayo kila baada ya miaka mitano wanafanyiwa tathmini, kulingana na mabadiliko ya kimazingira, teknolojia, uchumi, hali ya hewa na ikolojia.

Anataja miongoni mwa majukumu makubwa ambayo yako katika mpango mkakati huo, ni kuhifadhi na kuzilinda rasilimali za misitu na nyuki, zilizo katika hifadhi misitu ya taifa. Hapo anafafanua: "Kwa Kanda ya Ziwa, tunazo hifadhi za misitu zipatazo 24, sawa na hekta 415,000, ambazo tunahakikisha zinahifadhiwa, zinaendelea kulindwa, kuendelezwa, ili kuleta manufaa kwa kizazi cha sasa na kijacho kunufaika kiuchumi, kiikolojia na kimazingira."

Katika mustakabali wa utamaduni, anadokeza kuwa ndani ya hifadhi kuna shughuli zilizorithiwa zikiendelezwa hadi sasa, katika kukuza mila na desturi za jamii ya Kitanzania, zikileta faida za kiuchumi kwa njia za moja kwa moja na zisizokuwa za moja kwa moja kutoka katika misitu hiyo.

Mohamed anarejea katika uchumi, kwamba kuna manufaa ya kuwasaidia wananchi kupata mazao ya mbao kwa ajili ya shughuli za kijamiii, vilevile chakula, asali na dawa.

Pia, anataja suala la ikolojia ina manufaa kwa maisha ya binadamu na viumbe vingine, ikiismamia mazingira ya maisha. Hapo anafafanua kwamba mifumo ya kkolojia inagusa wanyama, mimea na wanyama, maji na hali ya hewa, huku kwa mwanadamu kuna mengi, maisha kwenda vizuri.

"Historia ya mistu na mwanadamu haiwezi kutenganishwa. Binadamu kwa miaka mingi, aliishi katika mistu, faida zake zilikuwapo tangu enzi na enzi, hivyo zitaendelezwa hadi leo," anaeleza Mohamed.

Anabainisha kuwapo faida zingine ambazo ni kuvuta hali ya hewa, kusimamia joto duniani, kupunguza hewa ya ukaa angani, kuvuta mvua ambayo ina manufaa makubwa kwa viumbe hai, mfano kilimo kinavyotegemea mvua.

Pia, Mohamed anataja uvuvi na mifugo nazo zina faida za kijamii na kiuchumi, kiikolojia wananchi wanazitambua, kuzithamini, akieleza TFS Kanda ya Ziwa inalenga kuhakikisha wananchi wanapata elimu sahihi ya mazingira na misitu yake, hata imeunda kitengo maalum cha kuelimisha umma umuhimu wa misitu.



Baadhi ya vitalu vya uzalishaji miche ya mifenesi, katika moja ya bustani ya TFS iliyopo jijini Mwanza.



Kamanda wa Wakala wa Huduma za Mistu Tanzania Kanda ya Ziwa, Bakari Mohamed. **PICHA ZOTE: ANTHONY GERVAS**

Anasema katika mikoa mitano inayosimamiwa na TFS Kanda za Ziwa; Mwanza, Simiyu, Mara, Kagera na Geita, katika wilaya zake kuna maofisa hifadhi wa misitu, wanaoelimisha umma, pia kulinda rasilimali za taifa, wakiwakumbusha wananchi kutambua faida hizo zisitoweke.

### BUSTANI ZA MICHE

Jukumu lingine, Mohamed analitaja ni kuhakikisha wananchi wanapewa miche bora ya miti ya kupanda, ili kutunza mazingira yao iwe faida ya baadaye, kwa umma.

Kamanda Mohamed, anaeleza kuwa zipo bustani za miche ya miti ya kupanda inayozalishwa kutoka kwenye bustani zao,zilizopo katika mikoa yao ya kanda ya ziwa,ili kuweza kutunza mazingira.

TFS katika kanda hiyo kwa sasa, ina jumla ya bustani 10 za kuzalisha miche ya miti mbalimbali ikiwamo ya matunda, miche ya asili ya vivuli, mbao inayotumika kwa ajili ya mahtaki ua kijamii, miche rafiki kwa mazingira katika vyanzo vya maji, ambayo inazuia mmomonyoko wa udongo.

Vilevile anataja miti ya kulinda ardhi, udongo wenye rutuba, kuzalisha mbolea za shambani kwa wananchi, hivyo bustani hizo huzalisha miche ya miti milioni 2.5 kwa mwaka, ambayo hugawiwa bure mwananchi mmoja mmoja kupanda, pia taasisi za umma na zisizo za umma katika maeneo mbalimbali yaliyoathriika.

Mohamed anaeleza, ni kawaida wananchi wanahimizwa kuchukua miti ya kupanda inayoendena na mazingira yao kiikolojia, aina ya udongo, hali ya hewa katika eneo husika, iwe inayohimili mvua nyingi na ukame.

Pia, anasema kuwapo ufugaji nyuki uliosheheni kwenye vikundi 80, ambavyo wanavipa elimu ya ufugaji na faida za asali. Anaeleza hadi sasa, soko la asali hiyo inapatikana katika nchi jirani za Rwanda, Burundi, Uganda na Jamhuri ya kidemokrasia ya Congo (DRC).

Vilevile kamanda huyo wa TFS anasema, huwa wanahakikisha kuwa na mashamba mahususi iliyotengwa kwa ajili ya kupandwa anayoiita 'miti ya kigeni', ambazo zina uharaka wa kukidhi mahitaji mazao ya mistu, inayosaidia kuzuia uharibifu wa misitu ya asili.

Anaeleza kuwa wanayo mashamba manne yaliyohifadhiwa kwa ajili ya kuvunwa mbao, ambayo yatakidhi mahitaji ya miti katika kukuza uchumi wa nchi, mtu mmoja moja. Anayataja na wilata il;iko katika mabano. Silayo (Chato); Buhindi (Sengerema); Rubale (Ukerewe); na Rubia iliyoko Biharamulo.

> “ Kuhusu ukanda aliko, anakiri kuwapo mabadiliko ya tabianchi, ambayo yamewaathiri kiuchumi wananchi katika kilimo, uzalishaji mali na kwenue uoto wa asili kutoweka.

Mohamed anataja maeneo yaliyopandwa miti ya kigeni kwa sasa hayazidi hekta 20,000, hivyo kila mwananchi anahamasishwa kuwa na shamba dogo la miti, itakayomnufaisha kiuchumi baadaye wakati wa kuvuna.

Shughuli zingine zinazofanywa, ni kuhudumia wafanyabisahara mazao ya misitu, wakishirikiana na halmashauri mbalimbali anazitaja ni kuhakikisha maeneo yote yanayohifadhiwa hifadhi za taifa yanalindwa, wananchi wakipewa elimu ya uendelezaji na utunzaji mazingira

### CHANGAMOTO ZILILOPO

Anasema changamoto iliyopo kwenye misitu ya asili ni uvunaji haramu, uvamizi wa mifugo kwa ajili ya malisho, akiwataka wananchi kushirikiana kufanya kazi za doria na mamlaka za wilaya husika kuwezesha kuzuia wahalifu wanaovamia maeneo hayo na kusababisha uharibifu wa misitu.

Mohamed anaeleza kuwa misitu ya asili kwa sasa ina uwezo mkubwa wa kurekebisha hali ya hewa duniani akitaja ni ufyonza hewa ya ukaa kwa kiwango kikubwa, vilevile kuhifadhi vyanzo vya maji vikiwaemo viumbe hai, akitumia mfano wa wanyama, wadudu, ndege na viumbe, vyote vikileta tija kiuchumi, kiikolojia pia kimazingira.

Anarejea kwamba madhara yanayoweza kutokea katika mistu ya asili inapovunwa holela, ni kukosekana mvua, uvuvi kuathirika, vyanzo vingi vya maji kukauka, kukumbwa na ukame, mifugo kuathirika kwa kukosa maji na malisho na hali mbaya za hewa kwa wakazi.

Kuhusu ukanda aliko, anakiri kuwapo mabadiliko ya tabianchi, ambayo yamewaathiri kiuchumi wananchi katika kilimo, uzalishaji mali na kwenue uoto wa asili kutoweka.

Rai yake Kamanda Mohamed, ni kwa viongozi wa ngazi mbalimbali za vijiji kuhakikisha wanainga mkono TFS, katika kutoa elimu ya kupiga vita uvamizi wa mistu, kwani wanafanya kazi kwa niaba yao kulinda rasilimali za nchi.

Pia, analalamika kuwapo uvamizi wa misitu kwa ajili ya kilimo, uchimbaji madini na shughuli mbalimbali za kibinadamu na mifugo, ikidhibitwa kuanzia na uelewa binafsi, itasaidia kuondoa kero ya kunyoosheana vidole.

MAZINGIRA

# SBL yawajibikia jamii kupitia 'Lengo la Sita SDG' maji imfikie mama Handeni

**Na Frank Monyo**

"Hadi Februari, 2022, hali ya upatikanaji wa maji safi maeneo ya mijini imefikia asilimia 86. Aidha, kati ya miradi 114 inayotekelezwa katika maeneo mbalimbali, miradi 40 imekamilika na kuanza kutoa huduma kwa wananchi wapatao 1,978,730 na miradi 74 ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji."

Hiyo ni kauli ya Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, wakati akitaja mafanikio ya serikali katika awamu iliyopo sasa, chini ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akisema utekelezaji wa miradi ya maji serikalini, kwa sasa ina dhamira ya kuhakikisha huduma ya maji mijini na vijijini inafika zaidi ya wastani wa asilimia 95 na 85, ifikapo mwaka 2025.

Hapo anawashukuru washirika wa maendeleo,wakiwamo nchi rafiki, taasisi na mashirika ya kimataifa, kwa kuendelea kuunga mkono juhudi za serikali kutoa huduma kwa wananchi.

Ikumbukwe maji safi na salama, afya bora, pamoja na mazingira sahihi ni sehemu ya ubora ni mahitaji ya msingi ya binadamu, pia yana umuhimu kwa viumbe wote wanaoishi duniani, hata visivyo na uhai.

Uhaba wa maji safi na salama, kimsingi ni chanzo cha uchafu wa mazingira, maradhi na chanzo cha migogoro, kama busara haitakuwapo kuvitunza. Inatajwa kuwapo ushahidi wa kitafiti, pale serikali na jamii, hazitasimama kidete kulinda, kutunza na kuendelezwa vyanzo vyake. Kimsingi, ni sehemu ya haki msingi za binadamu.

Hadi sasa upatikanaji wa maji safi na salama kwa wote bado ni changamoto, huku nchi zinazoendelea zikiathiriwa zaidi, Tanzania ikiwa sehemu yake. Hata ikirejewa, taarifa mojawapo ya Benki ya Dunia, inataja theluthi mbili ya Watanzania ndizo zinazopata huduma ya msingi ya maji.



Hali halisi ya shida ya maji vijijini wilayani Handeni. **PICHA: MTANDAO**

Ripoti zinathibitisha kutotosheleza huduma za maji na usafi (WASH), ikiwa ni kikwazo kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi, hali ambayo pia inaangukia mwitikio wa Umoja wa Mataifa (UN), unapokubali maji na usafi wa mazingira, kama eneo linalohitaji uangalizi, wakati wa kuandaa Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) mwaka 2015.

Hadi sasa dhana 'Maji na Usafi wa Mazingira' yako chini ya lengo la sita la SDG, linalotaka kuhakikishwa upatikanaji uendelevu. usimamizi wa maji na usafi wa mazingira kwa wote.

Mara nyingi, kutofikiwa na maji safi na salama, hata kuwa na athiri hasa kwa kinamama, ambao ndio wanaolazimika kutembea umbali mrefu kutafuta maji kwa ajili ya familia zao, ambayo katika sura ya pili, inabaki kuwa kikwazi kwao kushiriki shughuli za maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

### SBL YAINGILIA KATI

Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL), katika utaratibu wa uwajibikaji wa kampuni, imeamua kuwekeza katika mipango ya huduma za maji na usafi, hasa kwa wanawake wilayani Handeni, mkoani Tanga.

Mkurugenzi wa Uhusiano wa kampuni ya SBL, John Wanyancha, anataja nguzo mojawapo inayotumiwa na SBL, ni ushirikishaji, ikiwalenga wanawake kuwa kundi linaloonekana limesahaulika katika mradi huo, ni hatua ya kimkakati kuhakikisha kuna ushirikishwaji katika huduma za maji na usafi.

Wanyancha anasema, SBL imewekeza kiasi cha Sh.milioni 25 ikiwagusa zaidi ya watu 2,000 wanaotarajiwa kunufaika, wakiwamo wanawake na watoto.

Pia, anasema fedha hizo zitatumika kuwapa wanawake elimu inayohusiana na huduma za maji na usafi, pia ni akitaja ni mradi unaotekelezwa kwa ushirikiano na shirika la Water Aid, ukitarajiwa kuanza wiki ijayo eneo la Kwamaizi Kampene, kata ya Kideleko wilayani Handeni.

Mkurugenzi Wanyancha anafafanua: "Tuna shauku kubwa na mradi huu kwa sababu unagusa nguzo zetu mbili ambazo ni 'Maji ya Uhai'..."

Kwa mujibu wa Wanyancha, ni mradi mwendelezo wa maji wa Sh.milioni 380 unaotekelezwa wilayani Handeni. Anafafanua: "Mwezi uliopita tulianzisha mradi mkubwa wa maji huko Handeni, kwa kuanza ukarabati na ujenzi wa bwawa la maji kwa kushirikiana na Wizara ya Maji, pamoja na msaada na serikali ya mtaa wa Handeni.

"Baada ya hapo, tuliamua kimkakati kuanzisha mradi wa huu wa maji na usafi unaozingatia jinsia, ili kuwawezesha kundi lililotengwa huko Handeni na kwenye hili, sio wanawake tu kuendesha ajenda yetu ya ushirikishwaji, pia kuchangia kufikia lengo la sita la SDGs."

Anaongeza kuwa mradi wa Sh.milioni 25, una mana kwa wanawake eneo la Kwamaizi Handeni, kwamba watapata elimu inayohusiana na maji na usafi, hata kupata ufahamu wa kipengele cha fursa za ujasiriamali kwenye eneo hilo na uwekezaji.

Manufaa mengine yanatajwa ni kupatikana mafunzo juu ya ustadi na utunzaji bustani unaojali mazingira, piaa ujuzi wa usimamizi wa fedha. "Ili kufanya mpango huo kuwa endelevu zaidi, wanawake watapewa pesa za kununua mbegu za mazao mbalimbali ili kuwawezesha kununua zana ambazo kwa madhumuni ya kuwekeza katika huduma za maji na usafi".

## Chanjo aliyozindua Rais yajibu makubwa kimataifa, WHO ikimwaga pongezi

**INATOKA UK.11**

Mganga Mkuu wa Serikali, Profesa Tumaini Nagu, katika uzinduzi wa maadhimisho ya Wiki ya Chanjo Kitaifa yaliyofanyika kwenye uwanja wa Kwaraa mjini Babati, mkoani Manyara, anasema: "Hapa nchini mafanikio ya chanjo ni dhahiri kwa mfano tumefanikiwa kutokomeza ugonjwa wa ndui, magonjwa ya dondakoo, kifaduro, polio na pepopunda.

"Chanjo ni afua (nyenzo) muhimu katika kutokomeza magonjwa na kupunguza vifo hususani vya watoto wa chini ya miaka mitano. Chanjo pia hupunguza gharama kubwa ambazo familia zetu kwa ujumla ingetumia katika kutibu maradhi yatokanayo na magonjwa yanayozuilika kwa chanjo."

Anafafanua: "Nitoe msisitizo kuwa mtoto yeyote ambaye hajapata kabisa chanjo au hajakamilisha ratiba ya chanjo, ni hatari sana kwa afya yake kwa sababu anaweza kuambukizwa magonjwa na pia ana hatari ya kuwaambukiza wengine sababu hana kinga kamili ya mwili."

"Wiki hii ni mahususi katika kuhimiza familia kuwapeleka watoto wote wanaostahili kupata chanjo katika vituo vinavyotoa huduma za afya vya serikali na binafsi ili wapate chanjo," anafafanua.

Anataja mikakati ya Rais Dk. Samia, ni kuhakikisha huduma za afya hususani za chanjo inaendelea na zinaboreshwa

Kwa upande wake Dokta Nemes Iria ambaye ni Afisa WHO Afya ya Watoto na Chanjo, anatajaManyara ni mkoa ambao ulikuwa nyuma katika utaoaji wa chanjo lakini kwa ushirikiano na serikali ya mkoa wameanza kuzifikia jamii kwa kupeleka wataalamu huku wakiutumia kama mfano katika kupata matokeo chanya

WHO pia imeiorodhesha Tanzania kati ya nchi zilizofanikiwa zaidi Duniani katika utoaji wa chanjo mbalimbali tangu kuanzishwa kwa shirika hilo miaka 75, iliyopita kutokana na mipango thabiti ya serikali nchini.

WHO nchini inasema chanjo nchini Tanzania imekuwa zaidi kwa asilimia 2.8, kati ya Januari 2022 na Januari mwaka huu.



# Ujenzi tangi maji kumaliza kero maji

**Na Paul Mabeja,** CHAMWINO

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dodoma (DUWASA) imekamilisha mradi wa ujenzi wa tangi lenye uwezo wa kuhifadhi lita milioni 2.5 ili kukabiliana na tatizo la maji katika eneo la Chamwino Ikulu.

Mradi huo ulizinduliwa jana na Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, katika Kata ya Buigiri wilayani hapa, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya miaka 59 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

Akisoma taarifa ya mradi huo, Mkurugenzi Mtendaji wa DUWASA, Aron Joseph, alisema ujenzi wa tenki hilo umegharimu kiasi cha Sh.bilioni 1.12 na utaondoa tatizo la maji katika Wilaya ya Chamwino eneo ambalo iko Ikulu.

Alisema mahitaji ya maji katika eneo hilo ni lita milioni 3.6 na uwezo wa kuzalisha maji kwa siku hivi sasa ni lita milioni 4.4 kwa siku hali inayofanya eneo hilo kuwa na ziada ya maji kwa zaidi ya miaka 30 ijayo.

"Kukamilika kwa mradi huu kumefanya asilimia 87 ya watu wa wilaya ya Chamwino kuwa na uhakika wa maji na umeongeza upatikanaji wa maji kwa asilimia 55," alisema.

Alisema mradi huo ulikuwa umetengewa kiasi cha Sh. bilioni 2.5 lakini kutokana na kutumia mfumo wa 'Force Account' kimetumika kiasi cha Sh. bilioni 1.12 na kuokoa asilimia 50 ya fedha hizo.

Naye Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Nadhifa Kemikimba, alisema hali ya upatikanaji wa maji nchini kwa sasa ni asilimia 77 vijijini na asilimia 88 mijini.

Alisema asilimia 90 ya wakazi wa Jiji la Dodoma wanapata maji kwa njia ya mgao na mahitaji ya maji kwa siku ni lita milioni 133.4 huku uzalishaji ni lita milioni 67.8 kwa siku na hivyo kuwa na upungufu ni asilimia 54.

Katibu Mkuu huyo alisema ongezeko la mahitaji yam aji linakuwa kila mwaka na ili kukabiliana na hali hiyo DUWASA wanaendeleza jitihada za kuboresha huduma za maji ikiwamo kuchimba visima katika eneo la Nzuguni vitakavyo hudumia eneo la Nzuguni, Swaswa na Ilazo.

Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Abdallah Hassan Mitawi, alisema lengo la kuadhimisha miaka 59 ya Muungano kwa kufanya shughuli mbalimbali za maendeleo ni kushirikisha wananchi matunda ya Muungano.

# Hakuna korosho kuuzwa zikiwa ghafi

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imeazimia kuanzia msimu wa uzalishaji wa 2025/26 korosho zote kutoka Tanzania hazitauzwa tena zikiwa ghafi nje ya nchi.

Aidha, katika mwaka ujao wa fedha wa 2023/24, serikali itatenga Sh. bilioni 10 kwa ajili ya mradi wa ujenzi wa viwanda vikubwa vitatu vya kubangua korosho.

Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, alisema hayo jana jijini hapa kwenye kikao maalum cha wadau wa korosho kutoka mikoa yote inayozalisha zao hilo.

Alisema mfumo wa kuuza korosho ghafi unaikosesha nchi nafasi ya kupata faida kubwa ya fedha za kigeni,lakini pia unapunguza nafasi za ajira kwa vijana wa kitanzania.

Bashe alisema ili kufikia azma hiyo, vitajengwa viwanda vya kubangua korosho katika Halmashauri ya Nanyamba mkoani Mtwara, Manyoni mkoani Singida na Kongwa mkoani Dodoma.

Waziri huyo pia alitoa onyo kwa kampuni na mawakala wa pembejeo wanaojihusisha na kuuza bidhaa feki kuwa hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yao.

Pia alisema wakulima wengi nchini wamekuwa wakishindwa kuzalisha mazao muhimu ya kibishara kutokana na kufikiwa na pembejeo wakati ambao msimu wa kilimo umepita.

"Tumejipanga kuondoa tatizo hilo. Wizara imeandaa taratibu maalumu wa kuzichukulia hatua kali taasisi zote za fedha zitakazobainika kuhusika na ucheleweshaji huo ikiwa ni pamoja na kuwatoza faini mbalimbali.

"Inasikitisha sana kuona namna ambavyo uzalishaji wa Korosho nchini unazidi kudidimia wakati nchi yetu imebarikiwa kuwa na maeneo mengi yanayofaa kuzalisha zao hilo. Kwa mfano katika msimu huu matarajio yalikuwa ni kuzalisha zaidi ya tani 400,000 lakini tumeishia kuzalisha tani 180,000 tu," alisema.

Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Korosho, Francis Alfred, alisema bodi imejipanga kutekeleza programu mbalimbali za kuboresha uzalishaji na ubanguaji wa korosho nchini.

"Kwa kushirikiana na kituo cha TARI (Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania) Naliendele, tunatarajia kuendesha mafunzo mbalimbali ya kuwawezesha wakulima kuzalisha kwa kuzingatia taratibu za kiagronomia zinazoshauriwa na wataalam lengo likiwa kuanza kuzalisha angalau tani 51,000 kila mwaka kuanzia msimu ujao," alisema.




Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe akizungumza wakati wa ufunguzi wa kikao cha tathimini ya uzalishaji, ubanguaji na masoko ya korosho kwa msimu wa 2022/23 na maandalizi ya mwaka wa 2023/24, jijini Dodoma juzi. **PICHA: PETER MKWAVILA.**

# DC awa mbogo dhana potofu chanjo

**Na Elisante John,** SINGIDA

MKUU wa Wilaya ya Singida, Paskas Muragili, amekemea dhana potofu kuhusu chanjo zinazotolewa kwa kuwa hazina madhara na zinalenga kuwakinga watoto na magonjwa mbalimbali.

Kutokana na hali hiyo, amewataka wazazi na walezi wenye watoto wanaotakiwa kupata chanjo hizo kuondokana na fikra hizo.

Muragili aliyasema hayo jana wilayani hapa alipokuwa akizindua wiki ya chanjo kitaifa iliyoambatana na maadhimisho ya miaka 59 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar na uwekaji wa jiwe la msingi la zahanati ya kijiji cha Isomia, itakayohudumia wananchi 1,452.

Alisema ni umuhimu wa wazazi kuwapeleka watoto walio chini ya umri wa miaka mitano kupata chanjo zinazostahili na wasichana wenye umri wa miaka tisa hadi 14 ili kuwakinga na saratani ya mlango wa kizazi.

"Wananchi tusiwe na dhana potofu kwamba chanjo zinazotolewa zina madhara kwa watoto. Niwahakikishie zimefanyiwa utafiti wa kutosha na wataalamu waliobobea hata kabla ya kuingizwa nchini, hivyo hazina madhara yoyote," alisema.

Alisema wazazi hao wanapaswa kuzingatia maelekezo yanayotolewa na wataalamu wa afya kuhusu chanjo zinazotolewa.

Awali, akitoa taarifa ya ujenzi huo, Kaimu Mganga Mkuu wa Manispaa ya Singida, Dk. Hamis Yuna, alisema mradi huo ukikamilika utahudumia wajawazito na watoto wa kijiji hicho, na hivyo kupunguza vifo vya wajawazito na watoto na hadi sasa Sh.Milioni 60 zimetumika.

Alisema wananchi wamekuwa wakilazimika kutembea umbali mrefu wa kilomita sita hadi kijiji jirani cha Mwankoko ili kupata huduma za afya.





# Adaiwa kukutwa pori la akiba akitengeneza silaha za moto

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani hapa, linamshikilia mkazi wa Kambikatoto, Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya, Msabila Raulent (48), kwa madai ya kukutwa ndani ya Pori la Akiba la Rungwa, akiwa amejenga kambi akitengeneza silaha za moto aina ya gobore.

Mtuhumiwa huyo pia inadaiwa amekutwa akiwa ameanzisha mashamba ndani ya pori hilo akilima zao haramu la bangi, inayohatarisha uhai wa pori hilo pamoja na Hifadhi za Taifa za Ruaha na Katavi ambazo zinaunganishwa nalo.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi (ACP) Benjamin Kuzaga, alisema mtuhumiwa huyo alikamatwa katika msako uliofanywa kwa ushirikiano kati ya maofisa wa jeshi hilo na wa Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA) wa pori la Rungwa. Kuzaga alisema msako huo umetokana na taarifa za siri kutolewa na baadhi ya raia wema na ulipofanyika walikuta mtuhumiwa huyo akiwa amejenga kambi katikati na anaendelea na shughuli hizo.

Alisema katika upekuzi walikuta silaha mbili za moto aina ya gobore ambazo inadaiwa amezitengeneza kienyeji pamoja na vifaa mbalimbali ambavyo anavitumia kutengeneza silaha hizo.

"Mtuhumiwa tulimkuta na baruti, misumeno midogo, goroli ambazo anazitumia kama risasi, nyundo pamoja na vyuma vidogo vidogo ambavyo anavitumia kuunda silaha hizo," alisema Kamanda Kuzaga.

Pia alisema katika shamba alilolianzisha ndani ya hifadhi hiyo, kulikutwa kumepandwa miche 60 ya bangi, ambayo inaharibu mazingira na ikolojia ya pori hilo ambalo ni muhimu kwenye shughuli za uhifadhi.

Kamanda Kuzaga pia alisema wanamshikilia Elias Mwaimse (30), mkazi wa Mikoroshini, Wilaya ya Kyela, kwa tuhuma za kuvunja ofisi ya kampuni ya ulinzi ya AB & ANN Security Service Co. LTD na kuiba silaha aina ya shotgun yenye namba za usajili T. 26444 TZ CAR pamoja na risasi zake 17.

Alisema tukio hilo lilitokea Aprili 16, mwaka huu, na mtuhumiwa huyo alikamatwa siku sita mbele (Aprili 21) akiwa nyumbani kwake pamoja na silaha hiyo.

"Tulikuta ameificha silaha hii juu ya dari la nyumba yake ikiwa na risasi zote 17, tunaendelea kumhoji na baada ya mahojiano hatua nyingine za kisheria zitafuata," alisema Kamanda Kuzaga. Alisema watuhumiwa wote wawili wanaendelea kushikiliwa kwenye vituo vya polisi na watafikishwa mahakamani baada ya taratibu kukamilika.



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Benjamin Kuzaga akionyesha kwa waandishi wa habari juzi, baadhi ya silaha walizozikamata kwenye operesheni maalum iliyofanyika kati ya Aprili 15-23 mwaka huu, zilizokuwa zikitumika na wahalifu kutekeleza wizi .
**PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# 3,000 wenye ulemavu wapatiwa mafunzo kujikwamua kiuchumi

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

ZAIDI ya watu wenye ulemavu 3,000, wamepatiwa mafunzo ya ujasiriamali ili kuwawezesha kumiliki uchumi wao binafsi na kuondokana na utegemezi katika familia zao.

Mafunzo hayo yametolewa na Shirika la Furaha ya Wanawake Wajasiriamali Viziwi Tanzania, (FUWAVITA) kwa kushirikiana na wadau ambao wanawafundisha ujuzi wa aina tofauti ili kujiingizia kipato.

Mkurugenzi wa Shirika la FUWAVITA, Aneth Gerana, alisema wameamua kuanzisha mafunzo hayo ili kulisaidia kundi hilo kujikwamua kiuchumi kuliko ilivyo sasa ambapo idadi kubwa wamekuwa tegemezi kwa familia zao.

"Maono yangu ni kuona watu wenye ulemavu wanafanikiwa kibiashara, wanamiliki uchumi wao na vitu vya thamani, lakini ili tufike hatua hiyo lazima tuwapatie wenzetu elimu ya ujasiriamali ambayo itakuwa mwongozo wa kufanya biashara zao, na kupiga hatua za maendeleo," alisema Aneth ambaye ni kiziwi na msomi mwenye Shahada.

Alisema kupitia taasisi yake, ataendelea kuwafundisha watu wenye ulemavu, mbinu mbalimbali za kujikwamua kiuchumi, kupitia shughuli za ujasiriamali wanazozifanya.

Alisema anafanya hivyo, ili kulisaidia kundi hilo kuepukana na unyanyapa na kubaguliwa katika jamii ambao baadhi huwaona ni la watu walioshindwa maisha na kusahau kuwa, asilimia kubwa wamebarikiwa talanta mbalimbali. Katibu Mkuu wa Kanisa la Moravian, Jimbo la Kusini Magharibi, Israel Mwakilasa, alisema kwa kushirikiana na Shirika la FUWAVITA, wanaendesha mafunzo hayo ikiwa ni hatua za kulisaidia kundi hilo kujipatia kipato.

Alisema Kanisa lao lina kitengo cha kuwasaidia watu wenye ulemavu pamoja na kuwasomesha, kuwapatia misaada ya vyakula na malazi na wakati mwingine huduma za matibabu.

Akizungumza kwenye ufunguzi wa mafunzo hayo kwa niaba ya Mkurugenzi wa Jiji la Mbeya, Ofisa Maendeleo ya Jiji, Zena Kapama, alisema mafunzo hayo ni muhimu kwa watu wenye ulemavu, kwani yawasaidia kupata sifa ya kupata mikopo ya asilimia 10 inayotolewa na Halmashauri.

Katika mada yake, aliwasisitizia watu wenye ulemavu kujitahidi kufanya shughuli za kujiingizia kipato ili waweze kumiliki uchumi wao utakaowasaidia kuheshimika na kutimiza malengo yao.

Happy Sisina, mwenye ulemavu wa viungo ambaye anafanya biashara ya kuchoma mahindi mabichi eneo la Iwambi jijini hapa, alitaja miongoni mwa vikwazo vinavyowakabili ni ukosefu wa mitaji ya kukuza biashara zao.

Happy mwenye watoto watatu akiwalea mwenyewe baada ya kukimbiwa na mume wake, alisema anatamani kununua mzigo mkubwa wa mahindi lakini kikwazo ni mtaji na namna ya kuufikisha eneo lake la biashara.

## Asilimia 43 watoto mwaka 2022 hawajapewa vyeti vya kuzaliwa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

ASILIMIA 43 ya watoto wachanga waliozaliwa kati ya mwezi Januari na Desemba 2022 mkoani hapa, hawakuandikishwa na kupatiwa vyeti vya kuzaliwa kutokana na sababu mbalimbali, ikiwamo uelewa mdogo wa wazazi kuhusu umuhimu wa vyeti hivyo.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, aliyasema hayo jana wakati wa uzinduzi wa Kampeni ya Utoaji wa Vyeti iliyoanzishwa na serikali kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF).

Homera alisema katika kipindi hicho, watoto waliozaliwa walikuwa 82,212, lakini waliosajiliwa na kupatiwa vyeti vya kuzaliwa walikuwa 35,391, na hivyo kufanya zaidi ya watoto 46,800 kutoandikishwa na kupewa vyeti.

Alizitaja sababu ya watoto kukosa vyeti hivyo kuwa ni, pamoja na wazazi kutokujua umuhimu wake, kuchelewa kuwapatia watoto wao majina baada ya kuwazaa pamoja na mivutano kuhusu majina.

Alisema baadhi ya watoto huwa wanakosa vyeti hivyo kutokana na wanawake kutozijua taarifa za wazazi wenza na hivyo, kushindwa kuzitoa wakati wa kusajili, baada ya kujifungua kwenye kituo cha kutolea huduma za mama na mtoto.

Alisema watoto wakikosa vyeti vya kuzaliwa wanashindwa kupata baadhi ya huduma muhimu ikiwamo ajira na hata kupata vitambulisho mbalimbali kikiwamo cha cha taifa kinachotolewa na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA).

"Kumekuwa pia na tabia ya baadhi ya taasisi kutovitambua vyeti vya kuzaliwa ambavyo vinaandikwa kwa mkono wakidai kuwa, ni matangazo na siyo vyeti, sasa naagiza kuanzia leo vyeti hivyo vitambuliwe kama ilivyo kwa vile ambavyo vimechapishwa," aliagiza.

Ofisa Ustawi wa Jamii wa Mkoa wa Mbeya, Aika Temu, alisema vyeti vinavyotolewa kwa sasa ni kwa watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano, na kwamba vinatolewa bila malipo kutokana na kufadhiliwa.

Alisema vyeti hivyo vitatolewa kwa miezi mitatu mpaka mwezi Juni, mwaka huu, kwenye vituo vyote vya kutolea huduma za mama, baba na mtoto vya serikali na binafsi.

# Waziri apigilia msumari sheria ya mtoto

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Riziki Pembe Juma, amesema wizara hiyo imeshaipitia Sheria ya Mtoto ya Zanzibar ili kuhakikisha sheria hiyo inaendelea kumlinda mtoto na vitendo vyote vya udhalilishaji.

Waziri Pembe aliyasema hayo jana wakati akizungumza na Nipashe mjini Zanzibar kutokana na kuwapo kwa mijadala kutoka kwa baadhi ya watu kuwa umri wa mtoto upunguzwe badala ya kutambuliwa kisheria kuwa chini ya umri wa miaka 18 kwamba uwe chini ya miaka 14.

"WaKo wanaotaka kuwa umri wa mtoto upunguzwe wakidai kuwa idadi ya watoto wengi wanaozalilishwa ni wasichana kuazia miaka 14 hadi 18 huku wakisema watoto hao hujipeleka kwa wanaume," alisema.

Waziri Pembe alitafautiana na maoni ya watu hao na kusema umri wa mtoto utabaki kama ulivyoelezwa katika Sheria ya Mtoto kwa sababu mtoto chini ya miaka 18 anakuwa bado hajajitambua.

Alisema endapo umri wa mtoto utapunguzwa, watoto wa kike wataendelea kudhalilishwa.

"Watoto wote walio chini ya umri wa miaka 18, bado wana haki na nafasi ya kulindwa na katika hili serikali inaendelea kuwalinda kwa nguvu zake zote," alisema Waziri Pembe.

Pia alisema serikali inashirikiana na wadau mbalimbali katika kupinga vitendo vya udhalilishaji na kuwalinda wanawake na watoto na vitendo hivyo.

Pembe aliitaka jamii yote kusimama pamoja kuwalinda watoto wa jinsia zote kwa kuwa watoto wote wanadhalilishwa na kwa sasa wimbi kubwa liko kwa watoto wa kiume.

Alisema lazima kuwapo kwa ushirikiano wa pamoja katika kutokomeza vitendo hivyo jkwa sababu serikali pekee haiwezi kumaliza tatizo hilo.

"Tupambane katika kutokomeza ushoga, usagaji na vitendo vyote vya udhalilishaji kwa sababu bado baadhi ya watu wanaendelea kutukandamiza kwa kuunga mkono vitendo hivi ambavyo ni kinyume na maadili," alisema.

Kwa mujibu wa takwimu za udhalilishaji kwa Machi, mwaka huu, kutoka ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, matukio 155 ya udhalilishaji yameripotiwa Zanzibar.

Katika matukio hayo, ubakaji ni 69 na ulawiti 29 na kuingilia kinyume cha maumbile matukio sita. Waathirika wasichana waliobakwa ni 65, wavulana waliolawitiwa 24 na wasichana watano waliingiliwa kinyume cha maumbile.




Mawakala wa magazeti wakiyapanga baada ya kuwasili katika Bandari ya Malindi Mjini Unguja juzi yakitokea Dar es Salaam, kabla ya kuanza kuyasambaza katika maeneo mbalimbali. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# SMZ yaahidi mazingira bora ya kazi polisi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, amesema serikali zote mbili zitaendelea kuweka mazingira mazuri ya kufanya kazi kwa Jeshi la Polisi na vyombo vya ulinzi na usalama ili kuboresha utendaji katika kusimamia usalama wa raia na mali zao.

Amesema hatua hiyo inakwenda sambamba na kuenzi fikra na mawazo ya waasisi wa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar uliozaa Tanzania, Hayati Mwalimu Julius Nyerere na Hayati Abeid Amani Karume.

Hemed aliyasema hayo juzi katika ufunguzi wa ofisi ya makamanda wa polisi mikoa ya Kaskazini Unguja, Mahonda na Kusini Unguja, Tunguu, Zanzibar, ikiwa ni sehemu ya shamrashamra za maadhimisho ya miaka 59 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

Hemed alisema Muungano wa Tanganyika na Zanzibar unatokana na nia thabiti ya viongozi hao ambao ni waasisi wa taifa kwa kuzingatia uhusiano wa muda mrefu wa wananchi wa pande zote mbili.

Alisema Muungano huo unabaki kuwa wa kipekee Afrika na duniani kote sambamba na kuwataka wananchi kuendelea kuuenzi Muungano huo, kuutunza na kuulinda ambao ni tunu mojawapo inayoangaza maendeleo ya Watanzania.

Aidha, Hemed alisema kupitia Muungano huo, Tanzania ikishuhudia maendeleo makubwa na kuimarika kwa amani na utulivu nchini.

Pia alisema serikali zote mbili zinatambua kazi kubwa zinazofanywa na Jeshi la Polisi na kuna kila sababu ya kuwapatia mazingira mazuri pamoja na vifaa na zana za kisasa za kufanyia kazi.

Makamu huyo alieleza kuridhika kwake kuona fedha zilizotolewa kwa ajili ya mradi huo, zimetumika kwa mujibu wa thamani ya jingo, hivyo kulipongeza Jeshi la Polisi Kamisheni ya Zanzibar kwa kusimamia matumizi mazuri ya fedha za serikali na kuagiza kutunzwa kwa majengo hayo.

Pia alisema udhibiti mzuri wa matumizi ya fedha za serikali unatoa fursa ya kuendelea kujenga miradi mingine mipya ya kimaendeleo .

Kamishna wa Jeshi la Polisi Zanzibar, Hamad Khamis Hamad, alisema kwa kipindi cha miaka miwili, Kamisheni ya Polisi Zanzibar imepokea Sh. Bilioni 5.79 kwa ajili ya kukamilisha miradi iliyokuwa haijakamilika na ujenzi wa miradi mipya.

Pia alisema ujenzi wa majengo hayo mawili ya ofisi za makamanda wa mikoa, umegharimu Sh. bilioni 3.3 na kazi hiyo imefanyika kwa miezi tisa hadi kukamilika.

# Mke wa Rais apongeza huduma Aga Khan Z'bar

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKE wa Rais wa Zanzibar, Mama Maryam Mwinyi, amesema kufunguliwa kwa Hospitali ya Aga Khan visiwani Zanzibar kumeonyesha dhamira ya taasisi ya Aga Khan ya kuunga mkono juhudi za serikali katika kuimarisha ustawi wa afya kwa wananchi.

Aliyasema hayo jana wakati akifungua hospitali hiyo eneo la Malindi mjini Zanzibar, hafla ambayo ilihudhuriwa na viongozi mbalimbali wa serikali ya Zanzibar.

Alisema serikali ya Zanzibari inathamini juhudi za Aga Khan za kuendeleza miradi mbalimbali nchini ikiwamo ufunguzi wa hospitali ambayo itasaidia kutoa huduma za afya kwa wananchi wa Zanzibar na wageni wanaotembelea visiwani hapa.

"Hospitali hii ipo katika Mji Mkongwe wa Zanzibar ambao ni urithi wa dunia na unatembelewa na wageni kutoka mataifa mbalimbali duniani. Kuwapo kwake kutawahakikishia wageni uhakika wa matibabu bora wanapokuwa nchini," alisema.

Pia alielezea kuridhishwa na alichokiona baada ya kutembelea hospitali hiyo kwa kuwa na vifaa vya kisasa vya kutibu maradhi mbalimbali.

Mama Maryam, ambaye pia ni Mwenyekiti wa Taasisi ya Maisha bora, alisema uwapo wa hospitali hiyo utaimarisha juhudi za serikali za kujenga hospitali za wilaya na mikoa na kuifanya Zanzibar kuwa na upatikanaji wa huduma za uhakika kwa wananchi na kupunguza gharama zinazobebwa na serikali kusafirisha wagonjwa nje ya nchi.

Alisema dhamira ya serikali ya kutenga zaidi Sh. bilioni 100 kwa sekta ya afya inalenga kuhakikisha Zanzibar inakuwa na miundombinu bora ya kisasa ya afya, hospitali zenye hadhi na kuwawezesha watendaji wa sekta ya afya kufanya kazi zao kwa utaalamu na weledi.

Pia aliishauri Aga Khan kufikiria kuwekeza katika maeneo mingine yakiwamo masuala ya kiuchumi na urithi na kuishuru taasisi hiyo kupanua wigo na kuendelea kuiunga mkono Tanzania kwenye sekta mbalimbali hasa ya afya.

Balozi wa Ufaransa nchini Tanzania, Nabil Hajlaoui, aliihakikishia Tanzania kwamba nchi yake itaendelea kutoa msaada katika kuimarisha sekta ya afya ili kila mwananchi apate matibabu bora.

# Daraja la chini kuokoa wananchi ajali barabarani

**Na Elisante John,** SINGIDA

ZAIDI ya wanafunzi 1,600 wa Shule ya Msingi Kibaoni, Mahembe na wananchi, wataondokana na ajali za barabarani za mara kwa mara baada ya serikali kujenga kivuko cha chini kwenye eneo la Kibaoni, Manispaa ya Singida.

Kaimu Meneja wa Tanroads Mkoa wa Singida, mhandisi Yohannes Mbegalo, alisema ujenzi wa kivuko hicho chenye urefu wa mita 24.5, upana mita 4.6 na kimo mita 2.4, utakamilika Juni 22, mwaka huu na utagharimu Sh. milioni 427.8 na kuokoa maisha ya watu kila baada ya miezi mitatu.

Akizungumza mbele ya Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, wananchi na wanafunzi, alipokwenda kujionea maendeleo ya ujenzi, Mbegalo alisema, Wakala wa Barabara (TANROADS), aliamua kuchukua hatua ya kujenga kivuko cha chini cha waenda kwa miguu ili kuwezesha watumiaji kuvuka kwa usalama.

"Hapa licha ya kuwa na shule hizi, kuna wananchi wengi na makanisa, ambayo waumini huvuka kuwahi ibada na hatimaye hukutwa na kadhia ya kugongwa na magari, katika barabara hii ya Kintinku-Singida-Malendi, eneo la Kibaoni.....," alifafanua Mbegalo.

Baadhi ya wazazi, akiwamo Rachel Chaka, Theophil Macarius na Diwani wa Kata ya Misuna, Hamisi Kisuke, walisema kukamilika kwa kivuko ni nafuu kwa wanafunzi wanaopoteza maisha unaosababishwa na uzembe wa madereva, kushindwa kuzingatia alama za usalama barabarani.

Hata hivyo, wazazi hao wameiomba serikali, kujenga kivuko kingine cha juu karibu na eneo la Kibaoni, ambacho kitasaidia wananchi kuvuka nyakati za usiku ili kuepuka vibaka wanaovizia watu katika daraja la chini.

"Tumeelezwa kivuko hiki kitawekewa taa na kamera ili kudhibiti wezi, lakini sisi tunaomba tujengewe pia daraja la juu ili tuwe tunapita wakati wa usiku, kwa sababu hili hapa la chini sisi usiku itakuwa ni hatari, tutakabwa na vibaka," alisema Kiranga.

Akizungumza na wanafunzi na wananchi baada ya kukagua ujenzi wa kivuko hicho, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya miaka 59 ya Muungano, Mkuu wa Mkoa wa Singida, aliwataka kutumia kivuko hicho ili kuepuka ajali.

Alimtaka Wakala wa Barabara nchini (Tanroads), kuhakikisha amamsimamia vyema Mkandarasi aliyepewa jukumu la ujenzi wa mradi, aweze kukamilisha mapema zaidi ili wananchi wanufaike na kivuko hicho.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Ajira, Vijana na wenye Ulemavu), Prof. Joyce Ndalichako (kushoto), akijadiliana na jambo na Wafanyakazi wa Shirika la Kazi Duniani (ILO), Getrude Sima (kulia), Fanuel Maridadi (wa pili kulia) na Nasikiwa Berya walipokutana katika uzinduzi wa maadhimisho ya wiki ya mahali pa kazi Duniani, jijini Dodoma jana.
**PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## TACAIDS mbioni kukamilisha utafiti wa tano hali UKIMWI

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

TUME ya Kudhibiti Ukimwi Tanzania (TACAIDS) iko mbioni kukamilisha Utafiti wa Tano wa Hali ya Ukimwi huku takwimu za miaka 10 iliyopita zikionesha maambukizi mapya ya Virusi vya Ukimwi (VVU) yamepungua kutoka watu 110,000 hadi 54,000 kwa mwaka.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa jana ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, Mkurugenzi Mtendaji wa TACAIDS, Dk. Leonard Maboko, alisema uchumi bora wa nchi unategemea afya bora ikiwamo mapambano dhidi ya VVU ambayo Tanzania imepiga hatua kubwa kupunguza maambukizi hayo kutoka mwaka 2010 hadi 2021.

"Watazania bado tuna kila sababu ya kushirikiana katika kupambana na maambukizi ya VVU na Ukimwi, Tanzania inapiga hatua katika mapambano ya Ukimwi hasa kwa kuzingatia mambo matatu na tunapoelekea mwaka 2030, tuna malengo ya kutokomeza maambukizi mapya, vifo na unyanyapaa,"alisema.

Dk. Maboko alisema maambukizi hayo yamepungua kwa asilimia 50 na lengo la kupunguza vifo vinavyotokana na Ukimwi, akibainisha kuwa kwa mwaka 2010, kulikuwa na vifo 65,000 kwa mwaka na kwa sasa wanaofariki dunia ni 29,000.

"Suala la unyanyapaa mwaka 2013 tulikuwa tunaunyanyapaa asilimia 28 lakini mwaka 2021 unyanyapaa umeshuka na kufikia asilimia 5.5, hivyo tunakwenda vizuri kama nchi na hii ni takwimu ambayo inaonesha tunajitahidi," alisema.

Alihimiza kuwa kutokana na takwimu hizo, watanzania washirikiane ili kuendelea kuwa na afya njema.

Mkurugenzi huyo alisema wako kwenye mchakato wa kukamilisha kuchakata takwimu ili kuangalia hali ikoje kwa sasa ya ugonjwa huo.

# Watumishi DART wakumbushwa kujikinga VVU

**Na Joseph Mwendapole**

WATUMISHI wa Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART), wamekumbushwa kujiepusha na vitendo vinavyoweza kusababisha kupata maambukizi ya virusi vya Ukimwi (VVU).

Ushauri huo ulitolewa jana na Mkurugenzi wa asasi ya Tumaini Group, Onesmo Mwihava, wakati akizungumza na wafanyakazi wa Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART), kuhusu kujikinga na VVU.

Tumaini Group inafanyakazi na Mratibu wa Ukimwi Manispaa ya Ubungo, jijini Dar es Salaam kuelimisha umma kuhusu namna ya kukwepa maambukizi ya VVU.

Alisema Ukimwi bado upo na unaua hivyo watumishi hao wanapaswa kutumia njia mbalimbali kujikinga na kuhakikisha wanakuwa salama dhidi ya maambukizi hayo.

Aliwataka vijana kuachana na matumizi ya dawa za kuongeza nguvu wakati wa kujamiiana kwa kuwa zinachochea maambukizi mapya ya VVU.

Mwihava alisema hufanya kampeni mbalimbali kuelimisha vijana kuhusu VVU hasa wenye umri kuanzia miaka 13 hadi 25 na 25 mpaka 35 ambao takwimu zinaonyesha wako kwenye hatari ya kupata virusi hivyo.

Alisema vijana wamejihusisha na matumizi ya vitu vinavyosababisha msisimko kama pombe na dawa za kuongeza nguvu 'vumbi la kongo' wakati wa kufanya ngono.

Alisema dawa hizo zinaposisimua mwili zinasababisha wahusika kupata michubuko na kuongeza uwezekano wa kupata maambukizi mapya ya virusi hivyo.

"Huwa tunawashauri vijana wakapime na baada ya hapo wakapate ushauri na wale wanaogundulika kupata maambukizi waende moja kwa moja kupata dawa za kufubaza virusi vya Ukimwi ARVs)," alisema.

"Huwa tunawaambia vijana waachane na matumizi ya dawa hizi za kuongeza nguvu kwasababu zinasababisha michubuko wakati wa kijamiiana," alisema.

Alisema huduma ya dawa za ARV zimeongezwa kwa kuwa na vituo vingi na wote wanaobainika kuwa na VVU wanapaswa kuwahi mapema kuzitumia kwa kufuata ushauri wa wataalamu wa afya.

"Huduma ya dawa hizi inapatikana kirahisi sana na watu wakitumia vizuri wanaishi bila matatizo na hata hali ya unyanyapaa huwa haipo kwasababu tunaelimisha jamii kwamba kupata VVU sio mwisho wa maisha," alisema.

Alisema watu wanaopimwa na kubainika kuwa na VVU hawapaswi kukata tamaa badala yake wanatakiwa kusimama imara na kuangalia namna ya kuishi kama watu wengine kwenye jamii.

Mmoja wa watumishi wa DART, Yahaya Mgeni, alipongeza uongozi wa wakala kwa kuleta mafunzo hayo ambayo alisema yamewafumbua macho kuhusu changamoto mbalimbali za VVU.

"Tunaomba mafunzo kama haya yawe endelevu kwasababu Ukimwi bado upo na wananchi lazima wachukue tahadhari kwa hiyo mi vizuri kuwa tunakumbuswa kuchukua tahadhari mara kwa mara," alisema Yahaya.

# HABARI KIMATAIFA

## WHO yahadharisha kuhusu dawa ya kikohozi

**GENEVA,** Uswisi

SHIRIKA la Afya Duniani (WHO) limesema kwamba shehena ya dawa ya kikohozi yenye sumu ya India imepatikana katika visiwa vya Marshall na Micronesia, na kwamba zimekutwa na kiwango cha sampuli ambazo si salama kwa binadamu.

WHO ilisema kuwa sampuli zilizofanyiwa vipimo vya Guaifenesin TG syrup, iliyotengenezwa na kiwanda cha madawa cha Punjab QP Pharmachem Ltd, zinaonyesha kiwango kisichokubalika cha diethylene glycol na ethylene glycol.

Pia ilisema viungo vyote hivyo viwili ni sumu kwa binadamu na vinaweza kusababisha kifo iwapo mwanadamu atainywa.

Aidha, taarifa ya WHO haikuelezea wazi iwapo kuna yeyote aliyeugua kutokana na matumizi ya dawa hiyo.

Tahadhari hiyo ilikuja baada ya WHO kuhusisha dawa nyingine za maji za kikohozi zilizotengenezwa nchini India ambazo zilisababisha vifo vya watoto katika nchi za Gambia na Uzbekistan.

Mkurugenzi mkuu wa QP Pharmachem, Sudhir Pathak, aliiambia BBC kwamba kampuni ilikuwa imepeleka shehena ya chupa 18,346 katika mataifa ya Cambodia baada ya kupewa ruhusa ya kufanya hivyo.

Alisema kuwa hakujua iwapo bidhaa hiyo ilikuwa imefika katika Visiwa vya Marshall na Micronesia. **BBC**

**Kampuni ilikuwa imepeleka shehena ya chupa 18,346 katika mataifa ya Cambodia baada ya kupewa ruhusa ya kufanya hivyo.**

# Afrika yahimizwa kuipa kipaumbele sekta ya TEHAMA

**AFRIKA**

WADAU wa biashara na uchumi wamesema nchi za Afrika lazima ziongeze uwekezaji katika upatikanaji wa huduma ya intaneti kwa raia wake, kama zinataka kufikia kwa haraka maendeleo endelevu.

Kwa mujibu wa takwimu za bara la Afrika, biashara ndogo na zile za kati zinavutia uwekezaji wa takribani dola za Marekani bilioni tano kwa mwaka, huku asimilia 50 ya biashara hizo zikiwa Nigeria.

Mkurugenzi wa taasisi ya Smart Africa, Lacina Kone, alikiri kuwepo kwa changamoto ya nchi za Afrika kila mmoja kutaka kufanya jambo la maendeleo ya teknolojia peke yake, akitolea mfano kwamba kidole kimoja hakivunji chawa.

Kone, alisema kwa biashara ndogo na za kati kukua, nchi zinapaswa kuondoa vikwazo vya kibiashara na kutengeneza sera nzuri zitakazovutia uwekezaji barani Afrika.

"Utafiti unaonesha asilimia 90 ya biashara zilizoanzishwa hazikufa kwa sababu ya kifedha, ni kwa sababu ya kukosa mafunzo, uongozi na maendeleo ya biashara.

"Jambo la pili katika ngazi ya kidunia, pesa iko ili itumike, kwahiyo fedha kwangu mimi ni kama mvua na kama tunavyojua ili mvua inyeshe unahitaji vitu kadhaa kama mawingu na mawingu hayo ni mazingira rafiki ya sheria zitakazovutia ambazo nchi zetu lazima zifanyie kazi ili kumvutia muwekezaji," alisema Kone.

**Changamoto kubwa sana katika biashara hii ya teknolojia ni wapi utapata fedha katika hatua za awali kabisa, lakini pia wapi pakupata msaada wa ziada, mbali na ufadhili wa kifedha.**

Kuhusu ushiriki wa sekta binafsi, Kone alisema sekta hiyo kile ambacho haipendi ni kutotabirika kwa mazingira ya ufanyaji biashara na hasa kupitia teknolojia na kwamba ni lazima sera za nchi za Afrika zihuishwe kuleta urari wa kibiashara.

"Kama kweli tunataka sekta binafsi itumie fursa ya uwepo wa idadi ya watu bilioni moja na laki tano barani Afrika na tuna nchi 50 ambazo zote zina mifumo tofauti ya usimamizi, nadhani sote tunajua kwamba lazima tuwajibike katika kuhuisha mifumo yetu, kwahivyo nadhani kwangu mimi hii ndio changamoto kubwa," alisema Kone.

Aidha, alibainisha kuwa upatikanaji wa fedha sio shida kwa bara la Afrika, na kwamba Smart Afrika kwa kushirikiana na wadau wengine ikiwemo serikali ya Luxembourg na kampuni ya uwekezaji mitaji ya Bamboo Capital Partners, wameanzisha mfuko unaofahamiaka kama Block Smart Afrika, kuwawezesha wajasiriamali katika sekta ya teknolojia.

Winnie Mwangi, mkurugenzi wa uwekezaji kutoka kampuni ya Bamboo Capital Partners ya nchini Kenya, alisema wao wanaamini katika teknolojia kama mkombozi wa changamoto zinazoshuhudiwa barani Afrika na hasa kwenye sekta za Afya, elimu, kilimo na uhuishwaji wa kifedha.

Winnie, alisema mfuko huu ni wa kipekee kwa sababu ni ushirikiano kati ya sekta binafsi na umma na kwamba kwa sasa tayari serikali ya Ivory Coast imeshawekeza kwenye mfuko huu.

"Mwishowe utagundua unahitaji mwekezaji ambaye atakubali hatari ya biashara yenyewe hasa katika kipindi ambacho biashara inahitaji uwekezaji. Kwahiyo kuna tofauti kubwa sana kati ya uwekezaji wakati biashara inapoanza na baadae.

"Changamoto kubwa sana katika biashara hii ya teknolojia ni wapi utapata fedha katika hatua za awali kabisa, lakini pia wapi pakupata msaada wa ziada, mbali na ufadhili wa kifedha," alisema Winnie.

Vile vile, alisema bado kuna changamoto, idadi ndogo ya watu waliounganishwa na huduma ya intaneti hasa vijijini pamoja na matumizi hafifu ya teknolojia katika maeneo yaliyounganishwa bado ni shida kwa watu masikini, wanawake na biashara ndogondogo.

Pia inaelezwa kuwa ongezeko la hatari za kimtandao na kutokuwepo kwa ulinzi wa taarifa za watumiaji, zimeleta changamoto mpya kwa biashara, serikali na hata watu wa kawaida. **RFI**




Wanajeshi wakimbeba kwenye gari la wagonjwa raia wa Ugiriki aliyejeruhiwa mguu baada ya kuhamishwa kutoka Sudan, juzi. **PICHA: AFP**

# Wafungwa waachiliwa Sudan kwa kukosa chakula

**KHARTOUM,** Sudan

ALIYEKUWA waziri katika serikali ya Sudan, Ahmed Haroun, anayetafutwa na mahakama ya uhalifu ya kimataifa (ICC) kwa makosa ya uhalifu wa kivita, amesema kwamba ameachiliwa huru pamoja na wenzake, kutoka gereza la Kober kutokana na uhaba wa chakula.

Haroun alisema kwamba hali katika gereza la Kober lilipo nchini Sudan imekuwa mbaya katika siku za hivi karibuni.

Mtu aliyekamatwa kwa kufanya maandamano na kuzuiliwa katika gereza hilo, alisema kwamba wafungwa wameachiliwa huru baada ya kukosekana maji na chakula kwa muda wa wiki nzima.

Haroun alisema watu wengine ambao wameachiliwa huru ni pamoja na waliokuwa maofisa katika serikali ya aliyekuwa rais wa nchi hiyo Omar al-Bashir aliyeingia madarakani kupitia mapinduzi ya mwaka 1989 na serikali yake kuanguka mwaka 2019 kutokana na maandamano ya raia.

Aidha, inaelezwa kuwa mapigano yameendelea kushuhudiwa Sudan, jana saa chache baada ya kutangazwa muda wa kusitisha mapigano hayo huku kukiwa hakuna ishara ya pande zinazopigana kufanya mazungumzo.

Inaelezwa kuwa Jeshi la Sudan (SAF) na kundi la wapiganaji la (RSF) walikuwa wamekubaliana kusitisha mapigano kwa muda wa saa 72 kuanzia Jumanne, baada ya kufanyika mazungumzo yaliyoongozwa na Marekani na Saudi Arabia.

Lakini milio ya risasi ilisikika Jumanne jioni katika eneo la Omdurman, mojawapo ya miji ya Khartoum karibu na mto Nile ambapo jeshi la Sudan limetumia ndege zisizokuwa na rubani kulenga sehemu zinazoshikiliwa na RSF.

Mjumbe maalum wa umoja wa mataifa kwa ajili ya Sudan Volker Perthes, aliliambia Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa (UN) kwamba kuna ishara kwamba makubaliano ya kusitisha vita yanatekelezwa. **VOA**

# YANGA YAMTETEA AZIZ KI

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Yanga imesema kuwa mchezaji wake raia wa Burkina Faso, Stephane Aziz Ki, ana mchango mkubwa licha ya kudaiwa hana msimu mzuri na amekuwa na kiwango cha kupanda na kushuka.

**Afisa Habari wa Klabu hiyo, Ali Kamwe, amesema jana kuwa kwenye kikosi cha Yanga, hakuna kiungo mwenye mabao manane na 'assist' nne zaidi ya Aziz Ki, huku akisema kupanda na kushuka kwa mchezaji ni jambo la kawaida.**

"Kupanda na kushuka kunamtokea mchezaji yoyote duniani, kama inaweza kumtokea hata Cristiano Ronaldo au Lionel Messi, basi inaweza kumtokea mwingine yoyote. Tunavyojua Aziz Ki ni mchezaji ambaye anaweza kukupa matokeo chanya, au matokeo yasiyotarajiwa muda wowote ule kwenye mechi yoyote.

"Sitaki kuangalia sijui hajazoea mazingira au msimu wake wa kwanza, lakini alichokifanya tuna kila sababu ya kumpigia makofi kwa sababu amefikisha mabao manane na 'assist' nne, maana yake ameshachangia mabao 12 kwenye Ligi Kuu, achilia mbali mechi za kimataifa. Kwa hiyo licha ya kupanda kwake na kushuka, pamoja na kwamba mnasema hana msimu mzuri, lakini kwenye kikosi chetu hakuna kiungo mwenye namba nzuri kama zake," alisema Kamwe.

Alikumbusha kuwa kiungo huyo aliyesajiliwa msimu huu akitokea ASEC Mimosas ya Ivory Coast, ndiye anayeisababisha Yanga kucheza hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho barani Afrika kwa sasa kwa bao lake la ugenini alilolifungwa dhidi ya Club Africain ya Tunisia.

"Ni kiungo aliyeipeleka Yanga hatua ya makundi, sijui nyie mnamuangalia vipi, lakini sisi tunajua kuwa ni mmoja kati ya wachezaji wetu bora kabisa msimu huu huwezi kuacha kumtaja Aziz Ki," alisema.

Kumekuwa na maneno kwa wadau wa soka kuwa bado mchezaji huyo mpaka sasa hajaonyesha kiwango kile alichokuwa akionyesha alipokuwa klabu yake ya ASEC Mimosas kilichokuwa kikionekana msimu uliopita kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika, timu yake ikiwa kundi moja na Simba.

Baadhi yao wanasema kiwango chake kimekuwa ni cha kupanda na kushuka, akifanya vema baadhi ya mechi na nyingine akipotea.

Mchezaji hiyo alisajiliwa mwanzoni mwa msimu huu kwa usajili uliotia fora, na kuwa gumzo kubwa nchini.




Mgeni Rasmi, Diwani wa Kata ya Majengo wilayani Muheza Tanga, Mukadam Sabuni (Kushoto), kwa niaba ya Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Hamisi Mwinjuma 'Mwana FA', akikabidhi Ngao iliyoenda sambamba na zawadi ya Sh. 800,000, kwa timu ya soka ya TMF FC ya Muheza baada ya kuibuka mabingwa wa Kombe la Wazo Jipya Bakery Super Cup 2023 kwa kuifunga timu ya Damuni FC kwa mikwaju ya penalti 5-4 baada ya mchezo huo uliopigwa Uwanja wa Jitegemee, Muheza juzi, kumalizika kwa sare ndani ya dakika 90. Damuni FC ilizawadiwa Sh 400,000 kwa kumaliza nafasi ya pili huku mshindi wa tatu, Kwamkabara FC wakiondoka na Sh. 200,000. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# *JKT Queens yazidi kuinyima Simba Queens njia ubingwa*

**Na Adam Fungamwango**

MAAFANDE wa JKT Queens wanaonekana hawataki mzaha msimu huu na wamedhamiria kuwavua ubingwa Simba Queens, baada ya juzi ikiwa ugenini kutoa kipigo kizito cha mabao 6-0 dhidi ya The Tiger Queens.

Kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha, JKT Queens ilipata ushindi huo kwenye mechi ya raundi ya 25 ya Ligi Kuu ya Soka Wanawake inayoelekea ukingoni.

Kwa matokeo hayo, JKT Queens inafikisha pointi 37, ikicheza mechi 17, kushinda 11, na haijapoteza mechi yoyote mpaka sasa ikiongoza ligi hiyo ikibakisha mechi tatu tu kumaliza mechi zake msimu huu.

Iwapo itashinda mechi zote tatu, JKT Queens itatawazwa kuwa mabingwa na kuivua Simba Queens ubingwa ambao imekuwa ikiushikilia kwa misimu mitatu mfululizo.

Simba Queens ambayo jana ilitarajiwa kucheza dhidi ya Amani Queens, kama imeshinda inafikisha pointi 36 moja nyuma ya maafande hao na ili kuendelea kutetea ubingwa wao, inatakiwa kushinda mechi zote, huku ikiombea wapinzani wao watoke angalau mechi moja.

Timu ya Yanga Princess juzi kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam ilipata ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Ceasiaa Queens, yaliyowekwa nyavuni na Chioma Success na Cidalia Cuta.

Matokeo hayo yanaifanya timu hiyo kushika nafasi ya nne ikiwa na pointi 28, Ceasiaa ikibaki na pointi zake 18 ikiwa kwenye nafasi ya saba.

Katika Uwanja wa Chuo Kikuu cha Mkwawa, wenyeji Mkwawa Queens, walibabuliwa mabao 3-0 na Alliance Girls, matokeo ambayo yamewapeleka wageni hao kwenye nafasi ya tano kwa pointi 23, wenyeji wakiburuza mkia na huenda wakashuka daraja msimu huu, kwani wana pointi mbili tu.

## Kundemba FC haiihofii Mwembeladu FA

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya Kundemba FC imesema haina hofu na majirani zao Mwembeladu FC kuelekea mchezo wa Kombe la Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), maarufu FA Cup, unaotarajiwa kuchezwa Jumapili wiki hii katika Dimba la Amaan ikiwa ni hatua ya 16-bora ya michuano hiyo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa timu ya Kundemba FC, Ali Vua Shein, alisema anajua utakuwa mchezo mgumu kwa kuwa unakutanisha majirani wawili, hivyo kila timu itahitaji kumtambia mwenzake kwa kupata matokeo mazuri.

Alisema licha ya Mwembeladu FC kuwa Ligi ya Mkoa na wao kucheza Ligi Kuu, lakini bado mchezo huo utakuwa mgumu hivyo wanatakiwa kuivaa kwa tahadhari ili wafanikiwe kutinga robo fainali.

Alisema katika maandalizi ya mchezo huo, tayari kikosi chake kimeanza mazoezi mapema ili kujiandaa kikamilifu kwa mchezo huo wa Jumapili.

Awali, michuano hiyo ya FA Cup, ilipangwa kuendelea Mei 2, mwaka huu, lakini kamati ya Mashindano ya ZFF ambao ndio wasimamizi na waratibu wa michuano hiyo, wamerejesha nyuma ratiba hiyo ili kuepuka kuingiliana Kwa Karibu na ratiba ya Ligi Kuu Zanzibar.

## Rhino yaibamiza Lyon Daraja la II

**Na Adam Fungamwango**

HATUA ya nane bora ya Ligi Daraja la Pili Ngazi ya Taifa, iliendelea tena juzi kwenye Uwanja wa Azam Complex, wakati Rhino Rangers ilipotoa kipigo cha mabao 2-1 dhidi ya African Lyon.

Ilikuwa ni mechi ya Kundi B iliyoanza Jumatatu kwenye uwanja huo kwa ajili ya kusaka timu tatu zitakazopanda daraja la kwanza Championship msimu ujao.

African Lyon iliyoshuka daraja kutoka Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2020/21, ndiyo ilioanza kuziona nyavu za wapinzani wao likifungwa dakika ya 38 na Agili Ngoda na kudumu hadi mapumziko.

Kipindi cha pili, Rhino Rangers kutoka Tabora ambayo ilicheza Ligi Kuu msimu wa 2013/14, na ikasawazisha bao dakika ya 63 kupitia kwa Ramadhani Athumani, kabla ya Massawe Jacob kuandika bao la pili na la ushindi dakika saba kabla ya mechi hiyo kumalizika.

Mechi iliyofuatia iliyoanza saa 1:00 usiku ilikuwa ni kati ya TMA na Dar City zote za Dar es Salaam na mechi ikaisha kwa timu hizo kutoka suluhu ikiwa ni sare ya kwanza kwenye ligi hiyo msimu huu.

## ZISIKUPITE

### PHILLIPS ATAKIWA LIVER

KLABU ya Liverpool inataka kumsajili kiungo wa kati wa Manchester City, Kalvin Phillips, 27, msimu huu wa majira ya joto na mchezaji huyo wa kimataifa wa England, yuko tayari kuhama. ***(Star)***

### LUKAKU ATAJWA CHELSEA

CHELSEA itafanya mazungumzo na mshambuliaji wa Ubelgiji, Romelu Lukaku, 29, ambaye yuko kwa mkopo katika Klabu ya Inter Milan, na watamuuliza mchezaji huyo kama anataka kufufua soka lake la 'Blues' chini ya kocha mtarajiwa, Mauricio Pochettino. ***(Telegraph)***

### LAMPARD YUPO TAYARI

KOCHA wa muda wa Chelsea, Frank Lampard, yuko tayari kuzungumza na Mauricio Pochettino kuhusu kikosi hicho ili kusaidia mabadiliko yanayotarajiwa na Muargentina huyo. ***(Evening Standard)***

### PALHINHA AWINDWA EPL

KLABU za Tottenham Hotspur, Chelsea na Manchester United ziko tayari kumnunua kiungo wa kati wa Fulham na Ureno, Joao Palhinha, 27, msimu huu. ***(Football Insider)***

### ONANA KUTUA CHELSEA

CHELSEA ina nia ya kumsajili mlinda mlango wa Cameroon, Andre Onana, mwenye umri wa miaka 27, kutoka Inter Milan na wanaweza kumtumia kipa wao wa Hispania, Kepa Arrizabalaga, 28, kama sehemu ya mkataba huo. ***(Gazzetta dello Sport)***

### GRAVENBERCH KUBAKIZWA

KIUNGO wa kati wa Uholanzi, Ryan Gravenberch, 20, ambaye amekuwa akihusishwa na Liverpool, amesema anataka kucheza zaidi katika kikosi cha kwanza katika Klabu ya Bayern Munich msimu ujao na mchezaji huyo atasubiri kuona kitakachotokea katika klabu hiyo ya Ujerumani. ***(Voetbal International)***

### ARSENAL YAMFUATA NETO

ARSENAL inajipanga kufufua mpamngo wao wa kumnunua mshambuliaji wa Wolves kutoka Ureno, Pedro Neto, 23. ***(TeamTalk)***

### NEWCASTLE BAJETI KUBWA

KOCHA wa Newcastle United, Eddie Howe, atakuwa na bajeti ya uhamisho ya hadi pauni milioni 150 kutumia msimu huu wa majira ya joto. ***(Sun)***

### IBANEZ ATAJWA NEWCASTLE

KLABU ya Newcastle inamfuatilia beki wa kati wa AS Roma na Brazil, Roger Ibanez, 24. ***(Nicolo Schira)***

### MAXIMIN KUPIGWA BEI

NEWCASTLE United inatafakari uwezekano wa kumuuza winga wao, Mfaransa Allan Saint-Maximin, 26, msimu huu wa majira ya joto. ***(Football Insider)***

### LIVER, CHELSEA NA VUSKOVIC

LIVERPOOL na Chelsea zimeungana na Manchester City katika mbio za kumsajili beki wa kati wa Croatia, Luka Vuskovic, 16, kutoka Hajduk Split. ***(Daily Mail)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# ANCELOTTI: KICHAPO HIKI KITAIAMSHA REAL MADRID

**Ni baada ya kuduwazwa 4-2, asema mchezo ulikuwa mbaya kwenye safu ya ulinzi na...**

**MADRID,** Hispania

CARLO Ancelotti anatumaini kichapo cha aibu cha Real Madrid cha mabao 4-2 ugenini dhidi ya Girona Jumanne, kitakuwa sawa na simu ya kuwaamsha.

**Madrid haikuongoza pale kwenye Uwanja wa Montilivi, ikilala 2-0 ndani ya dakika 24 kutokana na mabao ya Taty Castellanos.**

Vinicius Junior alifunga bao moja, lakini Castellanos akaongeza mengine mawili kipindi cha pili kabla ya Lucas Vazquez kufunga bao la dakika za lala salama.

Castellanos amekuwa mchezaji wa kwanza katika karne hii kufunga mabao manne katika mchezo mmoja wa Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, dhidi ya Madrid, na kushindwa huko kunamaanisha Barcelona wanaweza kuongoza hadi pointi 14 kama walishinda mchezo wao wa jana, Jumatano.

Ingawa matumaini ya Madrid ya LaLiga yameshafifia, wametinga nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na na fainali ya Copa del Rey – na Ancelotti anatumaini kwamba kichapo hiki kitawarudisha kwenye morali. Alipoulizwa ikiwa kupoteza kunaweza kuwa simu ya kuwaamsha, Ancelotti alisema: "Ndio, inaweza kuwa.

"Ninasisitiza umuhimu wa kujitolea kwa ulinzi: tukiwa na hilo, tutashinda daima, na ikiwa sivyo, itatugharimu. Huo ndio ufunguo, ufunguo wetu, na leo (juzi) hatukuwa nao.


"Kati ya mechi saba zilizopita, tulicheza bila kuruhusu bao katika mechi sita na mchezo huu tuliruhusu mabao manne. Natumai wachezaji wangu wameelewa. Kama sivyo, nitarudia kila siku kwao."

"Ni ngumu, kwa sababu unapopoteza lazima iwe ngumu," aliongeza. "Mchezo ulikuwa mbaya kwenye safu ya ulinzi na hilo limekuwa jambo la msingi, kwa sababu tulifanya vizuri na mpira hasa mwanzoni.

"Lakini hatukuwa na nguvu katika mapambano, walitukamata kwenye mashambulizi ya kushtukiza mara mbili ... na kutoka hapo, kila kitu kilizidi kuwa kigumu."

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,107,4
MECHI KALI
TOTTENHAM
VERSUS
MANCHESTER UTD
1 | 2.60
X | 3.33
2 | 2.47
KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#,
CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom | m-pesa
BREAKING
airtel money
ZANTEL EZYPESA
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# NEWCASTLE YATENGA PAUNI MIL.150 ZA USAJILI



**LONDON,** England

KLABU ya Newcastle United imeripotiwa kupanga kutumia pauni milioni 150 katika dirisha lijalo la usajili, huku beki wa kushoto wa Arsenal, Kieran Tierney na winga wa Bayer Leverkusen, Moussa Diaby wakiwa kwenye orodha yao.

Tierney mwenye umri wa miaka 25, ni mchezaji wa kimataifa wa Scotland akiwa na mechi 37 za wakubwa kwa jina lake, lakini licha ya kucheza mechi 22 za Ligi Kuu msimu huu, ameanza michezo mitano tu.

Kocha wa Newcastle, Eddie Howe, ana nia ya kumrejesha Dan Burn katika eneo la ulinzi la kati na anamwona Tierney kuwa na uwezo wa kuchukua nafasi muhimu zaidi ya aliyo nayo pale Arsenal kwa sasa.

Wakati huo huo, winga wa Leverkusen, Diaby, mwenye umri wa miaka 23, ndiye anayepewa kipaumbele katika safu ya tatu ya mbele, akiwa amechangia mabao 14 na asisti 10 kwenye mechi zake 41 katika mashindano yote msimu huu.

Kwa mujibu wa The Sun, Howe ameambiwa atapewa pauni milioni 150 za kutumia, na anaamini pauni milioni 30 ni bei nzuri kwa Tierney kama beki wake mpya wa kushoto anayetarajiwa.

Diaby pia anahitajika na timu kadhaa, wakiwamo washindani wao wa Ligi Kuu, Arsenal na anatarajiwa kugharimu karibu pauni milioni 62.

Newcastle pia wanaripotiwa kumtaka mchezaji mwenza wa Diaby pale Leverkusen, Mitchel Bakker, ambaye ni beki wa kushoto mwenye umri wa miaka 23.



## Chelsea yapata pigo kwa James, Mount

**LONDON,** England

CHELSEA imepata pigo la majeraha mara mbili huku Reece James na Mason Mount wakitarajiwa kukosa msimu uliosalia, kocha wa muda, Frank Lampard alithibitisha hilo juzi, Jumanne.

James amecheza mechi 14 pekee za Ligi Kuu England kutokana na mfululizo wa matatizo ya utimamu wa mwili na alikabiliwa na tatizo jipya katika mechi ya mkondo wa pili wa kufuzu kwa robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya wiki iliyopita dhidi ya Real Madrid.

Mount amepatwa na tatizo la nyonga katika miezi ya hivi karibuni na sasa atafanyiwa upasuaji.

Lampard alipendekeza kuwa kuna uwezekano wa Mount kupatikana kwa mechi ya mwisho ya msimu ya Chelsea nyumbani kwa Newcastle hapo Mei 28, mwaka huu, lakini alitoa ubashiri wa hali ya chini wakati akizungumza kabla ya mchezo wa nyumbani wa ligi dhidi ya Brentford, Jumatano.

"Reece James hapatikani pengine kwa msimu huu, Mason Mount sawa," alisema Lampard.

"(Mount) ana uwezo w kuwa fiti kwa mechi y mwisho ya msimu hu lakini pengine sivyo. Kw hivyo ni wazi kwamba hi linakatisha tamaa kwetu.

"Ni pigo kubwa kwe sote kwa sababu ni wach zaji wakubwa. Reece a pata jeraha la msuli wa pa ambalo alilipata kweny mchezo wa Real Madri lakini tulilichanganua sil zilizofuata.

"Na Mason amekuwa r jeraha hili kwa muda mref bila shaka linajitambulish kwa muda mrefu.

## HABARI MICHEZO


65,397/-

## SUPA JACKPOT MECHI WIKI HII

### BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 29/04/23 | 19:00 | AS Roma vs AC Milan | 2.60 | 2.95 | 2.75 |
| 02. 29/04/23 | 19:30 | Schalke 04 vs Werder Bremen | 2.21 | 3.45 | 2.85 |
| 03. 29/04/23 | 20:00 | Velez Sarsfield vs CA San Lorenzo de Almagro | 2.30 | 2.80 | 3.00 |
| 04. 29/04/23 | 21:30 | Servette Geneva vs FC St. Gallen 1879 | 2.38 | 3.20 | 2.46 |
| 05. 29/04/23 | 21:45 | Torino FC vs Atalanta BC | 2.80 | 3.20 | 2.39 |
| 06. 29/04/23 | 22:30 | Gimnasia Y Esgrima La Plata vs CA Tigre | 2.70 | 2.95 | 2.33 |
| 07. 29/04/23 | 22:30 | Coritiba FC PR vs Sao Paulo FC SP | 2.95 | 3.10 | 2.34 |
| 08. 29/04/23 | 22:30 | Fortaleza EC CE vs Fluminense FC RJ | 2.60 | 3.15 | 2.60 |
| 09. 30/04/23 | 14:00 | Skovde AIK vs IK Brage | 2.70 | 3.10 | 2.25 |
| 10. 30/04/23 | 15:00 | Cadiz CF vs Valencia CF | 3.00 | 3.15 | 2.29 |
| 11. 30/04/23 | 15:30 | Glasgow Rangers vs Celtic Glasgow | 2.75 | 3.15 | 2.25 |
| 12. 30/04/23 | 16:00 | AFC Bournemouth vs Leeds United | 2.65 | 3.25 | 2.48 |
| 13. 30/04/23 | 16:00 | Clermont Foot 63 vs Stade Reims | 2.90 | 3.40 | 2.23 |
| 14. 30/04/23 | 18:30 | VfL Wolfsburg vs FSV Mainz | 2.26 | 3.40 | 2.85 |
| 15. 30/04/23 | 19:00 | Besiktas Istanbul vs Galatasaray Istanbul | 2.46 | 3.20 | 2.36 |
| 16. 30/04/23 | 19:00 | Ajax Amsterdam vs PSV Eindhoven | 2.20 | 3.25 | 2.75 |
| 17. 30/04/23 | 19:30 | Espanyol Barcelona vs Getafe CF | 2.31 | 2.95 | 3.15 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### ALHAMISI - 27/04/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:30 | 3802 | Sabah vs Selangor FC | 2.76 | 3.27 | 2.26 |
| 15:00 | 2745 | Ethiopia Electricity vs Wolkite City FC | 3.00 | 2.94 | 2.34 |
| 15:15 | 5985 | Kuala Lumpur vs Pdrm | 1.32 | 4.61 | 7.37 |
| 15:30 | 4384 | Spartak Subotica vs Javor Ivanjica | 2.01 | 2.98 | 3.60 |
| 16:00 | 2010 | Chippa Utd vs Kaizer Chiefs | 3.81 | 3.14 | 1.96 |
| 16:00 | 4008 | Reading U21 vs Colchester U21 | 1.59 | 4.34 | 4.14 |
| 16:00 | 4587 | Urartu vs Shirak Gyumri | 1.37 | 4.16 | 7.69 |
| 16:00 | 5823 | Penang vs Kuching FA | 1.46 | 4.11 | 5.54 |
| 17:00 | 1376 | FK Igman Konjic vs FK Sloga Doboj | 1.81 | 3.31 | 4.08 |
| 17:00 | 1685 | CA River Plate (Arg) vs Atletico Tucuman Reserve | 1.57 | 3.84 | 4.98 |
| 17:00 | 2434 | JS Kairouanaise vs ES Rades | 1.47 | 3.58 | 6.55 |
| 17:00 | 3076 | AS Mhamdia vs Avenir S Marsa | 4.13 | 2.89 | 1.92 |
| 17:00 | 3314 | Rosario Central Reserve vs CA Talleres de Cordoba Reserve | 1.81 | 3.41 | 3.93 |
| 17:00 | 5884 | Colon de Santa Fe Reserve vs Defensa Y Justicia Reserve | 2.22 | 3.10 | 3.05 |
| 17:30 | 1154 | Radnik Surduluca vs Radnicki Nis | 2.26 | 2.87 | 3.13 |
| 17:50 | 3747 | Al Seeb vs Sohar Club | 1.59 | 3.43 | 5.61 |
| 18:00 | 2897 | Duna Aszfalt Tvse vs MTK Budapest | 4.30 | 3.74 | 1.64 |
| 18:00 | 3733 | Soroksar vs Szentlorinc SE | 1.76 | 3.60 | 3.80 |
| 18:00 | 4000 | Viimsi JK vs Paide Linnameeskond | 1.27 | 5.99 | 8.55 |
| 18:00 | 4579 | Welayta Dicha FC vs Mekelakeya | 2.80 | 2.75 | 2.64 |
| 18:30 | 3843 | Moroka Swallows FC vs Maritzburg Utd | 2.10 | 2.93 | 3.66 |
| 18:45 | 3093 | Al Shabbab vs Al Ahli Manama | 2.41 | 2.95 | 2.89 |
| 18:45 | 4301 | Bahrain Club vs Al Hidd Club | 2.74 | 3.00 | 2.49 |
| 19:00 | 1095 | Sabayil vs Gabala | 4.26 | 3.43 | 1.74 |
| 19:00 | 1097 | AL Adalh vs Al Taawon | 4.25 | 3.77 | 1.75 |
| 19:00 | 1776 | Universitatea Cluj vs UTA Arad | 2.18 | 3.00 | 3.25 |
| 19:00 | 2312 | FCI Levadia Tallinn U21 vs FC Tallinn | 1.51 | 4.69 | 5.11 |
| 19:00 | 2324 | HNK Rijeka vs Lokomotiva Zagreb | 1.89 | 3.29 | 3.60 |
| 19:00 | 2960 | Pyunik Yerevan vs Ararat Armenia | 2.59 | 2.91 | 2.70 |
| 19:00 | 3049 | AL Tai vs Abha | 2.00 | 3.62 | 3.40 |
| 19:00 | 4428 | Borac Banja Luka vs Zeljeznicar | 1.78 | 3.31 | 4.24 |
| 19:00 | 4662 | Flora II vs FC Nomme United | 4.69 | 4.58 | 1.57 |
| 19:00 | 5655 | JK Tabasalu vs FC Elva | | 3.95 | 2.93 |
| 19:30 | 5264 | SV Rugenbergen vs TuS Dassendorf | 8.70 | 6.01 | 1.22 |
| 19:45 | 1101 | Kuopion Elo vs FC Vaajakoski | 2.69 | 3.52 | 2.25 |
| 19:45 | 4156 | Barcelona W vs Chelsea W | 1.17 | 6.01 | 12.44 |
| 20:30 | 1074 | Valencia vs Valladolid | 1.72 | 3.61 | 4.31 |
| 20:30 | 2990 | Villarreal vs Espanyol | 1.57 | 3.85 | 5.20 |
| 21:00 | 4117 | Corinthians SP U20 vs Botafogo RJ U20 | 1.55 | 4.00 | 4.89 |
| 21:00 | 4534 | Santos SP U20 vs Bahia BA U20 | 1.58 | 3.95 | 4.68 |
| 21:30 | 1048 | FC Luzern vs FC Winterthur | 1.48 | 4.30 | 5.67 |
| 21:30 | 2853 | FC Sion vs FC Basel | 3.57 | 3.57 | 1.90 |
| 21:30 | 4597 | Al Ittihad Jeddah vs Al Shabab Riyadh | 2.01 | 3.62 | 3.36 |
| 21:45 | 3609 | Everton vs Newcastle | 4.40 | 3.55 | 1.72 |
| 21:45 | 5579 | Southampton vs Bournemouth | 2.22 | 3.26 | 3.01 |
| 22:00 | 1397 | Rotherham vs Cardiff | 2.74 | 2.94 | 2.59 |
| 22:00 | 2819 | Fiorentina vs Cremonese | 1.37 | 4.66 | 7.83 |
| 22:00 | 5054 | Independente FC U20 vs Capivariano SP U20 | 10.00 | 5.80 | 1.15 |
| 22:15 | 4598 | Tottenham vs Manchester Utd | 2.60 | 3.33 | 2.47 |
| 23:00 | 5077 | Athletic Bilbao vs Sevilla FC | 1.75 | 3.50 | 4.30 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# GALINOMA MEMORIAL TOURNAMENT 2023 KUPIGWA JUMAMOSI LUGALO

**Na Mwandishi Wetu**

MASHINDANO ya Gofu ya Galinoma Memorial Tournament 2023, yanatarajiwa kufurukuta Jumamosi wiki hii katika viwanja vya Gofu Lugalo, Dar es Salaam, imeelezwa.

**Akizungumza na mwandishi wetu jijini Dar es Salaam jana, Alex Galinoma, ambaye ni mtoto wa Marehemu, Brigedia Generali Ernest John Galinoma, alisema enzi za uhai wa baba yao, alikuwa Mwenyekiti wa Lugalo Golf Club mpaka pale umauti ulipomkuta mwaka 2016.**

Alisema shindano hilo lilianzishwa na familia ikishirikiana na uongozi wa klabu hiyo ili kumuenzi marehemu na wengine waliotangulia kwa kusheherekea maisha yao huku wakiongeza ufahamu kwa kuwaleta karibu na kuhamasisha watu kujiunga na gofu hasa wanawake na watoto, ambayo ilikuwa ndoto ya marehemu.

"Alhamisi watacheza wasaidizi wa wachezaji (caddies), Ijumaa wachezaji wa kulipwa na Jumamosi watacheza watoto (juniors), pamoja na wachezaji wasio wa kulipwa (amateurs). Tunatarajia mwaka huu wachezaji wengi watajitokeza, wakiwamo watoto," alisema.

Aidha, alisema kutakuwa na kliniki ya gofu kwa watu wengine mbalimbali ili kujifunza mchezo huo na kwamba itakuwa kwa wote hata ambao hawajawahi kucheza gofu wanakaribishwa na hakutakuwa na kiingilio.

"Tunawashukuru wadhamini na wengine wote waliojitokeza kutuunga mkono mwaka huu ili kuendeleza mchezo huu kupitia shindano hili litakalofanyika kwa mwaka wa nne," alisema.



Brigedia Generali Ernest John Galinoma, enzi za uhai wake akicheza gofu. **PICHA: MAKTABA**

## Robertinho: Wydad hawataamini

INATOKA UK. 24

wa Ligi ya Mabingwa Afrika, ni rekodi kubwa kwetu na inatupa nguvu ya kuamini inawezekana.

"Tumeifunga timu kubwa nikiwa miongoni mwa wachezaji waliocheza dakika 90, ni rekodi kubwa kwetu bado tuna dakika nyingine 90 ngumu kuhakikisha tunatinga hatua inayofuata," alisema Mzamiru ambaye ametokea kuwa kipenzi kikubwa cha mashabiki wa timu hiyo.

Aliongeza kuwa maneno mengi yanayozungumzwa hawayapi nafasi, wanachokiangalia sasa ni namna watakavyojiandaa kuwakabili Wydad kwa dakika 90 ngumu kwao.

"Wachezaji tunautaka sana huu mchezo, na malengo yetu ni kucheza nusu fainali, tuna waheshimu wapinzani wetu na tutacheza kwa nidhamu kubwa ili kutafuta ushindi ugenini jambo ambalo linawezekana," alisema kiungo huyo.

Naye aliyekuwa Kocha wa Simba na sasa akiinoa KCCA FC ya Uganda, Jackson Mayanja, aliliambia gazeti hili jana kuwa anaimani na timu yake hiyo ya zamani kufanya vizuri katika mchezo huo wa marudiano dhidi ya Wydad.

## *Rais Samia atamani*

INATOKA UKURASA 24

mkubwa kwa sababu soka ni dakika 90.

Alisema wamefanikiwa kupata ushindi wa maboa 2-0 dhidi ya Rivers United ugenini na kwamba ni matokeo mazuri, lakini wanahitaji kuingia katika mchezo huo kwa nidhamu na tahadhari kubwa kwa sababu ya kutotaka ya mwaka 2021 kujirudia kwao.

"Jumapili tunaipeleka nchi nusu fainali ya Afrika, tuna matokeo ya mabao 2-0 mkononi, lakini bado tuna kazi kubwa mechi ya marudiano hatutaki kuona ya Jwaneng Galaxy ilivyowatoa wenzetu hapa nyumbani," alisema Kamwe.

Kamwe pia, alisema timu zote mbili [Simba na Yanga], kufika hatua ya robo fainali moja ya kitu kilichochangia ni pamoja na hamasa kutoka kwa Rais Samia kwa uamuzi wake wa busara wa kutoa Sh. milioni tano kwa kila bao linalofungwa na timu hizo kimataifa.

# Michezo

Alhamisi Aprili 27, 2023

Nipashe





Chelsea yapata pigo kwa James, Mount UKURASA 22

# Rais Samia atamani kuiona Yanga Vs Rivers Utd

## ●●● Asema akipata nafasi atatinga kwa Mkapa J'2, wahofu ya Jwaneng kwa Simba...

**Na Saada Akida**

WAKATI Klabu ya Yanga ikisema itachukua tahadhari zote katika mchezo wao wa marudiano wa Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Rivers United ya Nigeria utakaopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa Jumapili ili kuepuka yasije yakawakuta ya watani wao wa jadi, Simba msimu uliopita dhidi ya Jwaneng Galaxy ya Botswana, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan, amesema akipata nafasi ataungana na Watanzania kushuhudia mechi hiyo.

Msemaji wa Serikali, Gerson Msigwa, akikabidhi zawadi ya Sh. milioni 10 kwa Yanga jijini Dar es Salaam jana, kutokana na ushindi wao wa mabao 2-0 walioupata ugenini nchini Nigeria dhidi ya Rivers United, ikiwa ni utekelezaji wa ahadi ya Rais Samia kwa kila goli litakalofungwa na timu hiyo pamoja na Simba kwenye michuano ya kimataifa, alisema rais amewapongeza kwa ushindi huo na kuahidi bado fedha zipo waendelee tu kutikisa nyavu.

**"Leo (jana), nimekuja hapa kutoa pongezi za Rais Samia Suluhu kwa ushindi wa mabao 2-0 na kuwatakia kheri katika mechi ya marudiano dhidi ya Rivers United na kuendelea kuwasisitiza kutikisa nyavu kwa sababu fedha zipo.**

"Wachezaji wacheze kwa moyo kwa sababu wanaitangaza Tanzania na amesema kama ratiba zake zitaenda vizuri basi atakuwa sehemu ya Watanzania watakaoshuhudia Yanga ikimfunga Rivers United katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam na [timu ya] Tanzania kuwa sehemu ya zitakazocheza nusu fainali," alisema Msigwa wakati akikabidhi kitita hicho.

Aidha, akawapongeza wasemaji wa klabu hizo mbili kwa kuwa licha ya mechi kuchezwa uwanjani, lakini pia inachezwa mdomoni kwa sababu ya kuuzungumza mpira.

Alisema kitendo cha kutengeneza maneno vizuri, wanahamasika watu wengi ikiwamo mashabiki na viongozi wa serikali kujikita zaidi katika mpira na kuendeleza sera za Rais Samia katika sekta ya michezo.

Hata hivyo, licha ya Yanga kuwa na faida ya mabao 2-0 dhidi ya Rivers United ugenini, imesema wataingia uwanjani kwa tahadhari kubwa na hawataki kuona makosa kama ya Simba ya kuondolewa katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa msimu uliopita na Jwaneng Galaxy ya Botswana, yakitokea kwao.

Oktoba 17, 2021, Simba ikiwa ugenini nchini Botswana kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika raundi ya kwanza, iliibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya wenyeji wao, Jwaneng Galaxy, kabla ya Oktoba 24, mwaka huo kushangazwa katika mchezo wa marudiano Uwanja wa Benjamin Mkapa kwa kipigo cha mabao 3-1, hivyo matokeo ya jumla kuwa 3-3, lakini ikatupwa nje kwa faida ya bao la ugenini na kuangukia Kombe la Shirikisho.

Kutokana na Yanga nayo kupata matokeo kama hayo ya Simba ugenini, lakini yenyewe ikiwa ni kwenye Kombe la Shirikisho Afrika hatua ya robo fainali, imeshtuka na kusema itachukua tahadhari kubwa wakikumbuka kilichowakuta watani wao wa jadi.

Katika mchezo huo wa mkondo wa pili dhidi ya Rivers United ya Nigeria, Yanga inahitaji sare yoyote ama ushindi ili kutinga hatua ya nusu fainali.

Akizungumza na Nipashe jana, Msemaji wa Yanga, Ally Kamwe, alisema mechi yao ya marudiano itakuwa ni ngumu na ushindani

INAENDELEA UKURASA 23

## TUPIENI BADO ZIPO...




Msemaji wa Serikali, Gerson Msigwa (kulia), akikabidhi kitita cha zawadi cha Sh. milioni 10 kwa Afisa Habari wa Yanga, Ally Kamwe, jijini Dar es Salaam jana, ikiwa ni utekelezaji wa ahadi ya Rais Samia Suluhu Hassan, ya kutoa Sh. milioni tano kwa kila goli litakalofungwa na Simba na Yanga kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho Afrika. Yanga iliibuka na ushindi wa mabao 2-0 ugenini nchini ugenini Nigeria Jumapili iliyopita dhidi ya Rivers United. **MPIGAPICHA WETU**

# Robertinho: Wydad hawataamini

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

HUKU Kocha Mkuu wa Simba, Robertinho Oliveira akisema kikosi chake kiko tayari kwa ajili ya mechi ya mkondo wa pili wa Ligi ya Mabingwa Afrika hatua ya robo fainali itakayochezwa kesho saa 3:00 usiku kwa saa za Afrika Mashariki kwenye Uwanja wa Mohamed wa Tano dhidi ya Mabingwa Watetezi, Wydad Athletic Club nchini Morocco, kiungo 'tindo' wa timu hiyo, Mzamiru Yassin, amesema wao kama wachezaji wanaitaka sana mechi hiyo.

Akizungumza akiwa nchini humo, kocha huyo, amesema mbele ya wanahabari kuwa wachezaji wake hawana hofu na mechi hiyo kutokana na kwamba wengi wao ni wazoefu wa michuano ya kimataifa na wameshacheza mechi nyingi ugenini.

Robertinho alisema kwenye mechi ya kesho anachoamini ni mbinu zake ambazo amezitengeneza kwa wachezaji kuelekea mechi hiyo ingawa hakutaka kuzitaja hadharani, akiweka wazi kwamba zitaonekana uwanjani na kuwashangaza wapinzani wao.

"Ni mechi ngumu, tunacheza na mabingwa watetezi, lakini tunaamini kwenye mbinu zetu tulizokuja nazo, sitozitaja hapa, haitokuwa mechi rahisi, lakini nina kundi la wachezaji ambao ni wazoefu wa kucheza mechi na timu kubwa tena ugenini, na pia haitokuwa mara ya kwanza kuja kucheza hapa, tulishawahi kuwapo hapa kucheza na Raja Casablanca kwa hiyo wachezaji wangu wameshazoea mazingira ya hapa, utakuwa mchezo mzuri na mgumu pia," alisema Robertinho.

Hata hivyo, licha ya baadhi ya wadau wa soka nchini kuikatia tamaa Simba kushinda ugenini dhidi ya Wydad, Mzamiru amesema hawana muda wa kusikiliza mengi yanaowakatisha tamaa kuelekea mchezo huo wa marudiano na badala yake imani yao ni moja tu 'inawezekana'.

Simba imewasili juzi usiku mjini Casablanca tayari kwa ajili ya mchezo huo wa marudiano dhidi ya wenyeji wao, Wydad ikiwa na faida ya ushindi wa bao 1-0 walioupata Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam Jumamosi iliyopita na Mzamiru anasema umewaaminisha inawezekana na wanaamini watafikia lengo lao la kutinga hatua ya nusu fainali wanayoisaka zaidi ya miaka minne kwa sababu wachezaji wote wanaari na wanautaka vilivyo mchezo huo.

Alisema anatambua mchezo huo utakuwa mgumu na ushindani mkubwa kwa sababu wanahitaji kuendeleza ushindi walioupata nyumbani wanaulinda katika mchezo huo wa marudiano.

"Tutaenda uwanjani tukiwa na akiba ya ushindi wa nyumbani na kitendo cha kumfunga bingwa mtetezi

INAENDELEA UKURASA 23


9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042